# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

**DODOMA** **APRILI, 2018**

**YALIYOMO**


| | |
|---|---|
| *VIFUPISHO ........................................................* | *ix* |
| *DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA* | *xiii* |
| *Majukumu ya Wizara ...........................................* | *xiii* |
| *A. UTANGULIZI ................................................* | *1* |
| *B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2017/18 ...........* | *3* |
| *Usimamizi wa Elimu ya Sekondari ........................* | *7* |
| *Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ..........................................................* | *11* |
| *Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu ..........* | *12* |
| *Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ......* | *15* |
| *Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu .......* | *16* |
| *Usimamizi wa Rasilimali za Wizara ......................* | *18* |
| *SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA KWA MWAKA 2017/18 .........* | *20* |
| *Taasisi ya Elimu Tanzania ....................................* | *20* |
| *Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) .........* | *22* |
| *Baraza la Mitihani la Tanzania ..............................* | *22* |
| *Mamlaka ya Elimu Tanzania ................................* | *24* |
| *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ...............................................................* | *26* |
| *Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ........................* | *28* |
| *Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) ............................................................* | *30* |
| *Bodi ya Huduma za Maktaba .................................* | *32* |

*Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu* .... 33
*Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania* .............................. 34
*Tume ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH* ........ 36
*Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania* .................... 38
*Vyuo vya Elimu ya Juu* .......................................... 42
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania* ............................ 42
*Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi* ............................ 43
*Chuo Kikuu cha Ardhi* ............................................ 44
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* .............................. 45
*Chuo Kikuu cha Dodoma* ........................................ 46
*Chuo Kikuu cha Mzumbe* ....................................... 48
*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo* ....................... 49
*Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili* ............................................................. 52
*Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa* ............ 53
*Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam* ..... 54
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere* ...... 55
*Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya* ....... 56
*Chuo cha Ufundi Arusha* ....................................... 57
*Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam* ....................... 59
*Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha* ........................................ 60
*UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO* ..................................................... 62
*UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18* ............. 62

*Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu - EP4R)* ........................................................ 62
*Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya KKK* 65
*Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu* ..................... 66
*Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu* ............ 67
*Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu* ................ 69
*TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)* ... 70
*C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA 2018/19* ............................................... 73
*Kuendeleza Elimu ya Msingi kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu* ............................................. 73
*Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo Katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi* .................................. 74
*Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi* .... 75
*Kuainisha Mahitaji ya Nchi Katika Ujuzi na Kuuendeleza* ........................................................ 76
*Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu* .................................................. 77
*Usimamizi wa Elimu ya Msingi na Sekondari* ....... 78
*Usimamizi wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi* ............................................. 79
*Usimamizi wa Masuala Mtambuka katika Elimu* ... 80

*Usimamizi wa Elimu Maalum ................................ 81*
*Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ........................................................ 81*
*Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu .......... 82*
*Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ...... 83*
*Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu ....... 84*
*Usimamizi wa Rasilimali za Wizara ....................... 85*
*URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA ............................................ 86*
*Taasisi ya Elimu Tanzania ...................................... 87*
*Baraza la Mitihani la Tanzania ............................... 88*
*Mamlaka ya Elimu Tanzania ................................. 89*
*Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ........................ 90*
*Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ... 91*
*Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ........................ 93*
*Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ......... 93*
*Bodi ya Huduma za Maktaba ................................. 94*
*Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu .... 95*
*Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ............................. 96*
*Vyuo vya Elimu ya Juu ........................................... 98*
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ............................ 98*
*Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ............................ 99*
*Chuo Kikuu cha Ardhi ........................................... 99*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam .............................. 101*
*Chuo Kikuu cha Dodoma ....................................... 102*
*Chuo Kikuu cha Mzumbe ....................................... 103*
*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ....................... 104*

*Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili* ........................................................... 105
*Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa* ............. 107
*Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)* ........................................................ 108
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere* ...... 109
*Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya* ....... 110
*Chuo cha Ufundi Arusha* ....................................... 113
*Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam* ....................... 116
*Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha* ......................................... 117
*Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia* ............................. 118
*Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH* ......................................................... 119
*Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania* ................... 120
*MALENGO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2018/19* ................. 123
*Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu* .......... 123
*(Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu)* ............................................................... 123
*Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK* ............. 125
*Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu* .................... 126
*Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu* ............ 126

*Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu ................ 127*
*Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni ................................................ 129*
*Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP) .......................................... 130*
*Mradi wa TANZIS (Tanzania Innovation Systems) ................................................................ 130*
*TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18) ... 132*
*D. SHUKRANI ..................................................... 132*
*E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19 ............................................................ 134*

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACE** | African Center of Excellence |
| **ADEM** | Agency for the Development of Educational Management |
| **ANFED** | Adult and Non Formal Education |
| **ATC** | Arusha Technical College |
| **CBA** | Competence Based Assessment |
| **CBET** | Competence Based Education and Training |
| **CKD** | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| **CODESRIA** | Council for the Development of Social Science Research in Africa |
| **COSTECH** | Commision for Science and Technology |
| **DfID** | Department for International Development |
| **DIT** | Dar es Salaam Institute of Technology |
| **DLRs** | Disbursement Linked Results |
| **ENMRA** | Elimu Nje ya Mfumo Rasmi |
| **EP4R** | Education Program for Results |
| **ESDC** | Education Sector Development Committee |
| **ESDP** | Education Sector Development Plan |
| **ESMIS** | Education Sector Management Information System |

| | |
|---|---|
| **ESPJ** | Education and Skills for Productive Jobs |
| **EWW** | Elimu ya Watu Wazima |
| **FDC** | Folk Development Colleges |
| **GPE** | Global Partinership in Education |
| **HESLB** | Higher Education Student's Loans Board |
| **IGAs** | Income Generating Activities |
| **INTEP** | Integrated Training for Entrepreneurship Promotion |
| **IPOSA** | Integrated Program for Out of School Adolescent |
| **JESR** | Joint Education Sector Review |
| **JIRCAS** | Japan International Research Centre for Agricultural Sciences |
| **KKK** | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| **LANES** | Literacy and Numeracy Education Support |
| **MASW** | Masters of Arts in Social Work |
| **MCED** | Masters of Community Economic Development |
| **MCHAS** | Mbeya College of Health and Allied Sciences |
| **MIVARF** | Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support |
| **MMEM** | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |

| | |
|---|---|
| **MTUSATE** | Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia |
| **MUHAS** | Muhimbili University of Health and Allied Sciencies |
| **MUST** | Mbeya University of Science and Technology |
| **NACTE** | National Council for Technical Education |
| **NECTA** | National Examinations Council of Tanzania |
| **OR-TA-MISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **SEQUIP** | Secondary Education Quality Improvement Program |
| **SIDA** | Swedish For International Development Agency |
| **SSDL** | Secondary Standard Dosimetry Laboratory |
| **SSMP** | Sustainable Solar Market Packages |
| **STU** | Sayansi, Teknolojia na Ubunifu |
| **SUA** | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| **SWASH** | School Water Sanitation and Hygiene |
| **TCU** | Tanzania Commission for Universities |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TESP** | Teacher Education Support Program |
| **TLDs** | Thermolumiscent Dosimeter |

| | |
|---|---|
| **TWG** | Technical Working Group |
| **UDSM** | University of Dar es Salaam |
| **UIMS** | University Information Management System |
| **UNAIDS** | United Nation Programme on HIV and AIDS |
| **UNESCO** | United Nations Educational Scientific and Cultural Organization |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **VETA** | Vocational Education and Training Authority |
| **WHO** | World Health Organizations |

## DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

**Dira:** *Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa.*

**Dhima:** *Kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.*

### Majukumu ya Wizara

*Kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa tarehe 22 Aprili 2016, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloj ia inatekeleza majukumu yafuatayo:*

(i) *Kutunga na kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi;*

(ii) *Kuendeleza Elimumsingi kwa kutoa ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu;*

(iii) *Kusimamia uendelezaji wa mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;*

(iv) *Kusimamia mfumo wa Tuzo wa Taifa;*

(v) *Kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na*

*kuuendeleza;*

(vi) *Kuweka viwango vya taaluma ya Ualimu;*

(vii) *Kusimamia ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule;*

(viii) *Kusimamia huduma za machapisho ya Kielimu;*

(ix) *Kutegemeza/kuimarisha utumiaji wa Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati;*

(x) *Kuendeleza wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;*

(xi) *Kuratibu na kusimamia Utafiti na Ubunifu katika fani za Sayansi, Hisabati na Teknolojia;*

(xii) *Uendelezaji wa rasilimali watu na uongezaji tija ya watumishi walio chini ya Wizara; na*

(xiii) *Kuratibu shughuli za Idara, mashirika, wakala, programu na miradi iliyo chini ya Wizara.*

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2017/18. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2018/19.

2. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu. Kwa heshima na taadhima napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuiongoza Nchi yetu vyema na kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Vile vile, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa usimamizi mzuri wa shughuli za kila siku za Serikali na kunipatia Miongozo na Maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi katika hii Wizara. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali

Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb) na Makamu Mwenyekiti Juma Nkamia (Mb) kwa kuendelea kunipa ushirikiano mzuri na kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi, busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza mijadala ndani ya Bunge letu Tukufu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuchukua fursa hii pia, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kwenye uchaguzi mdogo akiwemo Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Siha), Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia (Kinondoni), Mheshimiwa Damas Daniel Ndumbaro (Songea Mjini), Mheshimiwa Justine Joseph Monko (Singida Kaskazini) na Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Longido).

6. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utelekezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/18 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 na maombi ya Fedha zitakazowezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yaliyopangwa.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2017/18

7. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2017/18 ulizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 – 2020/21, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, pamoja na Sera zinazohusu Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

### Bajeti Iliyoidhinishwa Katika Mwaka 2017/18

8. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,337,348,364,000.00** katika mafungu mawili tofauti, yaani Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia) na Fungu 18 (Tume ya Taifa ya UNESCO) ambalo nitaelezea utekelezaji wake baada ya Fungu 46.

**Bajeti Iliyoidhinishwa ya Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia)**

9. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,336,685,241,000.00** kwa Fungu 46 ambapo **Shilingi 419,843,419,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 916,841,822,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

10. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi 1,005,731,159,774.73** sawa na asilimia 75 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na kwa Miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo **Shilingi 321,824,364,822.48** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **77** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, **Shilingi 683,906,794,952.25** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **75** ya Bajeti ya Maendeleo.

11. **Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizotumika hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 zilikuwa ni **Shilingi 749,795,644,445.99** sawa na asilimia **75** ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 281,874,146,587.30** zilitumika kwa Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 467,921,497,858.69** zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo.

## KAZI ZILIZOTEKELEZWA MWAKA 2017/18 KWA FUNGU 46

**12. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inatekeleza majukumu yake kupitia Idara, Vitengo na Taasisi kama ilivyofafanuliwa katika majukumu ya Wizara. Naomba nianze kwa kutoa taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/18 kama ifuatavyo:

**Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**13. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kusimamia Ithibati ya Shule kwa lengo la kutoa vibali vya kuanzisha na kuendesha shule vikiwemo; ujenzi wa shule, umiliki na umeneja wa shule na usajili wa shule. Jumla ya shule 154 zilizokidhi vigezo zimesajiliwa kati ya shule 171 zilizoomba usajili. Mchanganuo wa shule zilizosajiliwa unajumuisha Shule za Awali na Msingi 123 na Sekondari 31. Vile vile, Wizara imetoa vibali vya kuongeza Tahasusi za masomo kwa Shule 37 za Sekondari kati ya 50 zilizoomba. Wizara pia imetoa vibali vya ujenzi wa shule mpya 112 zilizotimiza vigezo kati ya maombi 167 yaliyopokelewa. Vibali hivyo vilitolewa kwa shule za Sekondari 19, Awali na Msingi 63, Awali pekee 29 na Chuo cha Ualimu kimoja.

**14. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kusimamia Uthibiti Ubora wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, ili kuhakikisha kuwa viwango vya utoaji wa elimu vilivyowekwa vinazingatiwa na kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu bora. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule pamoja na zana za utekelezaji wa Kiunzi. Aidha, imeendesha Mafunzo elekezi ya mfumo mpya wa utekelezaji wa kazi za Uthibiti Ubora wa Shule ambayo yalifanyika kwa Wathibiti Ubora wawezeshaji wa kitaifa 51 watakaoendesha mafunzo elekezi kwa Wathibiti Ubora wa Shule katika ngazi ya Kanda na Wilaya; na

(ii) imefungua ofisi mpya 5 za Uthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya za Songwe, Kigamboni, Ubungo, Chalinze na Ushetu kwa lengo la kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya hizo.

**Usimamizi wa Elimu ya Sekondari**

15. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kitengo cha Elimu ya Sekondari kimeratibu na kusimamia ushiriki wa wanafunzi wa Kitanzania katika mashindano ya Uandishi wa Insha za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Wanafunzi wa Sekondari kwa lengo la kuwajengea uwezo katika uandishi na ujenzi wa hoja. Katika mashindano ya Afrika Mashariki mwanafunzi *Michael Msafiri Nyaruga* wa Kidato cha Nne (2017) kutoka Shule ya Sekondari Kibaha – Pwani, alishika nafasi ya Kwanza. Aidha, katika mashindano ya insha ya nchi za SADC wanafunzi wawili (2) wameingia katika 10 bora. Wanafunzi hao ni *Neema Steven Mtwanga* (Kidato cha Sita) wa Shule ya Sekondari Lugalo - Iringa na *Fadhila Sanga* (Kidato cha Nne) wa Shule ya Sekondari Nasuli iliyopo Wilaya ya Namtumbo - Ruvuma.

**Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi**

16. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) kukamilisha Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2017-2021 (*Education Sector Development Plan – ESDP)* pamoja na Mpango wa Utekelezaji (*Operational*

*Plan*) wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu; na

(ii) kukamilisha na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Kanuni za Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu zitakazoimarisha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

**Kuendeleza Elimumsingi kwa Kutoa Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu**

**17. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imetoa mafunzo ya matumizi ya TEHAMA kwa jumla ya Wakufunzi 250 na Wathibiti Ubora 25 kwa lengo la kuimarisha ujuzi na maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) imetoa mafunzo ya Elimu ya Awali kwa jumla ya Wakufunzi 38 na Wathibiti Ubora 25 kwa lengo la kuimarisha ujuzi na maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(iii) imedahili jumla ya wanachuo wapya 7,454 wa Mafunzo ya Ualimu wakiwemo 4,368 wa Astashahada (Cheti) na 3,086 wa Stashahada. Hii imefanya jumla ya

wanachuo wote waliopo katika Vyuo vya Ualimu kuwa 20,236.

**Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vimedahili jumla ya wanafunzi 5,050 na kuwapa mafunzo katika fani za Upishi, Kilimo na Ufugaji, Ufundi Umeme wa Majumbani, Ufugaji Samaki na Nyuki, Ususi na Ufumaji, Usindikaji wa Vyakula na Matunda, Ushonaji, Uchomeleaji Vyuma, Umekanika, Kompyuta, Useremala, Uashi, Utengenezaji Mapambo, Ujasiriamali, Uendeshaji Hoteli na Umeme wa Magari.

**19.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya tathmini ya hali ya miundombinu katika Vyuo vyote 55 vya Maendeleo ya Wananchi. Tathmini hiyo imebaini uchakavu wa miundombinu, vifaa, mitambo na upungufu wa watumishi katika Vyuo hivyo. Aidha, Wizara inafanya upembuzi yakinifu wa miundombinu ambapo kwa sasa taarifa ya upembuzi inaandaliwa na itakamilika tarehe 4 Mei, 2018. Baada ya kupata taarifa hiyo Wizara itafanya ukarabati na ujenzi katika vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi katika Awamu ya Kwanza.

**20. Mheshimiwa Spika**, Kupitia ushirikiano na wadau wa Elimu ambao ni *Karibu Tanzania Organization*, *Master Card Foundation, Aflatoun* na Ubalozi wa Sweden nchini Tanzania, Wizara imeweza kuandaa programu mbili ambazo ni *Elimu Haina Mwisho na Mpira Fursa.* Programu hizi zimejikita katika kutoa elimu ya stadi za maisha na ujasiriamali kwa wasichana nje ya mfumo rasmi wa elimu na pia kufungua fursa ya ajira kwa mchezo wa mpira wa miguu. Kiasi cha Dola 100,000 zimetengwa kwa kipindi cha miaka minne (4) na tayari kwa mwaka 2017-18 wasichana 569 wamepata mafunzo hayo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, katika Programu ya *Mpira Fursa* ambapo kiasi cha Paundi za Uingereza 550,000 zimetengwa kutumika kwa kipindi cha miaka minne (4), jumla ya wasichana 523 kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii 27 wamepata mafunzo ya kuwawezesha kushiriki katika mchezo wa mpira wa miguu.

**Kuainisha Mahitaji ya Nchi katika Ujuzi na Kuuendeleza**

**21. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi *(Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)* imekamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi *(Skills Development Fund)* kwa

lengo la kutoa ruzuku kwa vyuo na taasisi za mafunzo katika ngazi zote pamoja na waajiri wa sekta binafsi ili kufadhili programu za mafunzo zinazozingatia mahitaji ya soko la ajira. Programu hizo zinahusisha sekta sita za kipaumbele zilizoainishwa katika mpango mkakati wa taifa wa kuendeleza ujuzi (*National Skills Development Strategy*), ambazo ni kilimo, TEHAMA, nishati, ujenzi, uchukuzi na utalii. Katika Awamu ya Kwanza mfuko unatarajiwa kutoa ruzuku kwa programu za sekta ya Kilimo. Taratibu za kuwapata wanufaika zipo katika hatua za mwisho na sherehe ya kuwatangaza washindi itafanyika kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2018.

**Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**22. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu taratibu za kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa miundombinu, majengo, vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) imeratibu maandalizi ya awali ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Simiyu, Geita na Rukwa; na

(iii) imeratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara na umeme kwenye eneo kitakapojengwa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera ambapo barabara na nguzo za umeme vimefikishwa hadi eneo la ujenzi wa Chuo.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**23. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini. Aidha, masuala ya Ithibati na Uthibiti wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini yanatekelezwa kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeratibu Skolashipu 135 za wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Nje ya Nchi zikiwemo 10 za Jumuiya ya Madola (Uingereza 8 na New Zealand 2); Urusi 12 na China 113. Aidha, imekamilisha mchakato wa maombi ya Skolashipu za Jumuiya ya Madola kwa mwaka wa masomo 2018/19 na kupendekeza waombaji 26 ambao majina yao yamewasilishwa kwenye Baraza la Skolashipu za Jumuiya ya Madola kwa hatua zaidi. Vile vile, imekamilisha mchakato wa kupokea maombi na kupendekeza majina 30 kwa ajili ya Skolashipu za Serikali ya Hungary

kwa mwaka 2018/19;

(ii) imefadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kutekeleza mkataba wa ushirikiano wa kiutamaduni kati ya Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;

(iii) imeratibu kusainiwa kwa mkataba wa mahusiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Hungary ili kuwezesha upatikanaji wa fursa za masomo 30 (5 Uzamivu, 15 Uzamili na 10 Shahada za Kwanza) kila mwaka kwa kipindi cha miaka Mitatu;

(iv) imefuatilia maendeleo ya udahili na uandikishwaji wa wanafunzi katika taasisi za Elimu ya Juu pamoja na maendeleo ya utoaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(v) imefuatilia zoezi la udahili wa wanafunzi unaofanyika moja kwa moja kwenye Taasisi za Elimu ya Juu; na

(vi) imeratibu uanzishaji na usimamizi wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (*African Center of Excellence (ACE II*)).

Katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kuna Vituo viwili ambavyo ni Kituo cha Umahiri cha Afrika cha Ubunifu wa Mbinu za Kudhibiti Wadudu na Wanyama Waharibifu kwa Kutumia Teknolojia ya *Bio-Sensor* (*African Center of Excellence for Innovative Rodent Pest Management and Bio - Sensor Technology (IRPM&BTD))* na Kituo cha Kusini mwa Afrika cha Kutafiti Magonjwa yanayoambukiza (*Southern African Centre for Infectious Diseases Surveillance (SACIDS))*. Aidha, katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela kuna vituo viwili ambavyo ni Kituo kwa ajili ya Utafiti wa Miundombinu na Nishati Endelevu (*Water Infrastructure and Sustainable Energy Centre for the Futures)* na Kituo cha Ushirikiano cha Utafiti na Maendeleo ya Kilimo na Ufundishaji *(Collaborating Centre for Research, Evidence, Agricultural Advancement and Teaching Excellence and Sustainability (CREATES))*. Vituo hivyo vimeanzishwa ili kuongeza fursa za masomo katika ngazi ya uzamili na uzamivu; na hivyo kuongeza idadi ya wataalamu wenye umahiri katika kukabiliana na changamoto za kijamii na kiuchumi.

**Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

24. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu la kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini, Wizara katika mwaka 2017/18 imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imefanya makubaliano na Serikali ya Finland katika mradi wa kuendeleza ubunifu nchini wenye thamani ya Euro 12,773,000, ambapo Serikali ya Tanzania inachangia Euro 3,823,000 na Serikali ya Finland inachangia Euro 8,950,000. Mradi utatoa msaada wa kitaalamu kwa wabunifu pamoja na nafasi ya kushindania fedha za kuendeleza ubunifu. Mradi huu utachochea ushirikiano kati ya Wanataaluma, Wabunifu na wenye viwanda; na

(ii) imefanya makubaliano na Serikali ya Finland katika mradi wa Awamu ya Pili wa Kuendeleza Ubunifu katika nchi za Kusini mwa Afrika ambapo Tanzania inashiriki kwa mara ya kwanza. Nchi nyingine ni pamoja na Afrika Kusini, Botswana, Namibia na Zambia. Mradi huu unalenga kuboresha ushirikiano wa kikanda katika ubunifu pamoja na mifumo ya ubunifu ya nchi wanachama ili kuongeza mchango wa ubunifu

katika biashara na maendeleo kwa ujumla. Mradi huu wa Awamu ya Pili wa Kuendeleza Ubunifu katika nchi za Kusini mwa Afrika una thamani ya Euro 12,550,000 ambapo wabunifu kutoka nchi wanachama watashindanishwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa taasisi kibunifu ili ziweze kuwasaidia wabunifu kupata ushauri wa kitaalamu. Vile vile, mradi huu utaimarisha uwezo wa Wajasiriamali kifedha ili waweze kuingiza bidhaa zao sokoni na kuweka mazingira rafiki kwa shughuli za wabunifu.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu**

**25. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu la kusimamia na kuendeleza Rasilimaliwatu, kwa mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya uhamisho wa watumishi 43 toka Dar es Salaam kuja Dodoma na kufanya jumla ya watumishi waliohamishiwa Dodoma kuwa 273 kati ya watumishi 328 wanaotakiwa kuhamia Dodoma. Uhamisho huu umelenga kutekeleza Mpango wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Mkoani Dodoma;

(ii) imetoa mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (*Open Performance Review and Apraissal System* – OPRAS) kwa watumishi wote wa Makao Makuu ya Wizara, Vyuo **35** vya Ualimu, Ofisi 11 za Uthibiti Ubora wa Shule Kanda na Ofisi za Uchapaji (Press A, Press B na Tabora). Lengo la mafunzo ni kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi kwa kuweka malengo ya pamoja baina ya mwajiri na mwajiriwa na kujipima kwa kipindi cha nusu mwaka na mwaka;

(iii) imetoa Mafunzo Elekezi (*Induction Course*) kwa watumishi wapya 89 ili kuwajengea ufahamu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maadili ya Kazi katika utumishi wa umma kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi;

(iv) imeratibu na kuendesha Mafunzo ya Awali ya Mfumo wa Kupokea, Kutunza na Kusambaza Nyaraka za Ofisi (*E-Office*) kwa watumishi 20 wa Masijala na Maafisa 02. Mafunzo yalilenga kuwawezesha watumishi wa Wizara kuanza kutumia mfumo huu ili kuleta ufanisi, kupunguza gharama na kuongeza kasi ya mawasiliano katika ofisi; na

(v) kuratibu uhakiki wa vyeti vya elimu na taaluma kwa waombaji wa kazi ya Ualimu kwa ajili ya kujaza nafasi **3,033** za walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Kilimo na Biashara katika shule za Serikali kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa walimu wa masomo hayo.

**Usimamizi wa Rasilimali za Wizara**

**26. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha udhibiti na usimamizi wa rasilimali za Wizara, katika mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) kukagua matumizi ya fedha za Mpango wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (*Literacy and Numeracy Education Support - LANES)* katika mikoa 10 na Halmashauri 20 ili kuona kama fedha zinazotumwa na Wizara zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali;

(ii) kukagua matumizi ya fedha za Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) katika shule 50 zilizo katika Halmashauri 22 ili kuona kama kazi zilizotekelezwa zinathamani ya fedha zilizotumika;

(iii) kukagua mapato, matumizi na usimamizi wa mali katika vyuo 6 vya Ualimu ili kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali yanakusanywa kikamilifu na matumizi yanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali;

(iv) kuthaminisha mali za Wizara katika makao makuu ya Wizara, Vyuo 35 vya Ualimu, ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za Kanda 11 na Wilaya 160 ili kutambua na kupata thamani halisi ya mali za Wizara;

(v) kukagua matumizi ya fedha za Mpango wa Lipa kwa Matokeo (EP4R) katika makao makuu ya Wizara na Shule za Sekondari; na

(vi) kutoa mafunzo ya menejimenti ya viashiria hatarishi (*Risk Management*) kwa watumishi 243 walioko makao makuu ya Wizara pamoja na taasisi zake. Katika mafunzo hayo vihatarishi vinavyoweza kuisababisha Wizara kutofikia malengo yake viliorodheshwa na kuwekewa mikakati ya udhibiti. Aidha, matokeo ya ukaguzi uliofanywa yameiwezesha Wizara kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani itakayoisaidia kufikia malengo iliyojiwekea.

## SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA KWA MWAKA 2017/18

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi, Wakala na Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyo chini ya Wizara, vinawajibika katika kuchangia usimamizi na hatimaye kufanikisha utoaji wa elimu bora nchini. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

### Taasisi ya Elimu Tanzania

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Elimu Tanzania katika kipindi cha mwaka 2017/18, imetekeleza yafuatayo:

(i) kuandika Vitabu vya Kiada vya masomo 7 ya darasa la IV. Vitabu hivyo ni vya masomo ya Hisabati, Sayansi na Teknolojia, Maarifa ya Jamii, Uraia na Maadili, *English, French* na Kiswahili;

(ii) kuboresha vitabu vyote vya kiada aina 17 vya Darasa la I – III vilivyotakiwa kufanyiwa mapitio. Jumla ya nakala 8,450,000 za vitabu vilivyopitiwa zimechapishwa na kupelekwa shuleni;

(iii) kutathmini miswada ya vitabu vya ziada 108 kutoka kwa makampuni/watu binafsi ambapo miswada 17 ilipitishwa kwa masharti ya kufanyiwa marekebisho

madogo; miswada 47 ilipitishwa kwa masharti ya kufanyiwa marekebisho makubwa na miswada 44 ilikataliwa kwa kutokidhi vigezo vya ubora;

(iv) kuboresha Mihtasari ya masomo ya Kidato cha I-IV na V-VI kwa Mtaala wa mwaka 2005 na 2009 ili kuendana na wakati;

(v) kutafsiri Moduli za Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Lugha ya Kiswahili na kuhariri Moduli za Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali;

(vi) kupokea na kufanyia tathmini vitabu vya ziada 120 kutoka kwa watu na makampuni binafsi;

(vii) kufanya utafiti kwa ajili ya kukusanya taarifa, maoni na mapendekezo ya kuboresha Mtaala wa Elimu ya Ualimu Ngazi ya Cheti katika mikoa 10 ya Tanzania Bara, ambayo ni Mbeya, Njombe, Mara, Mtwara, Kagera, Dodoma, Tabora, Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro; na

(viii) kuhariri na kuboresha zaidi moduli za mafunzo ya uendelezaji walimu kazini ili kuimarisha umahiri wa walimu katika kufundisha na kujifunza.

### Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)

**29.** **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kipindi cha mwaka 2017/18 imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili wanafunzi 2,873 katika programu za Astashahada, Stashahada na Shahada. Jumla ya wanafunzi wote wanaoendelea na masomo katika programu zinazotolewa kwa njia ya kawaida na Masafa ni 4,175 ambapo wanawake ni 2,116 sawa na 51% na wanaume ni 2,059 sawa na 49% ya wanafunzi wote;

(ii) imekamilisha ujenzi wa uzio wa kiwanja cha TEWW katika Mkoa wa Rukwa na kuandaa Mchoro wa jengo la ofisi katika mkoa wa Kagera; na

(iii) kusajili jumla ya vituo 104 vinavyotoa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi ili kuongeza fursa ya elimu ya sekondari kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi.

### Baraza la Mitihani la Tanzania

**30.** **Mheshimiwa Spika**, Baraza lina majukumu ya kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi na Sekondari, Ualimu Ngazi ya Cheti na Stashahada na Mtihani wa Maarifa. Katika

kipindi cha mwaka 2017/18 Baraza la Mitihani Tanzania limetekeleza yafuatayo:

(i) limeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Jumla ya watahiniwa 1,192,655 wa Darasa la Nne walisajiliwa ambapo watahiniwa 1,158,499 sawa na asilimia 97 walipimwa; na jumla ya watahiniwa 521,759 wa Kidato cha Pili walisajiliwa ambapo watahiniwa 486,742 sawa asilimia 93 walifanyiwa upimaji huo;

(ii) limeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi na Kidato cha Nne mwaka 2017. Jumla ya watahiniwa 916,885 wa Elimu ya Msingi walisajiliwa ambapo watahiniwa 909,950 sawa na asilimia 99 walifanya Mtihani huo; na jumla ya watahiniwa 385,802 wa Kidato cha Nne walisajiliwa kufanya Mtihani ambapo watahiniwa 374,938 sawa na asilimia 97 walifanya Mtihani huo;

(iii) limesajili jumla ya watahiniwa 76,789 watakaofanya Mtihani wa Kidato cha Sita Mei 2018;

(iv) limesajili jumla ya Wanachuo 9,895 ambapo kati ya hao 8,848 ni wa ngazi ya Cheti na 1,047 ni wa ngazi ya Stashahada ambao wanatarajia kufanya mitihani Mei, 2018; na

(v) limenunua mashine ya pili ya kufungia mitihani (*Poly wrapping machine*) na mashine ya rangi ya uchapaji mitihani (*Full Colour Printing Machine*) ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha usalama wa mitihani.

**Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**31. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imefanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 8 za walimu zinazoweza kuchukua walimu 6 kila moja katika shule za Sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu kufikika kwa ajili ya kuanza ujenzi. Nyumba hizo zitakapokamilika zitakuwa na uwezo wa kuchukua walimu 48 kwa wakati mmoja;

(ii) imetoa jumla ya shilingi milioni 700 kama mkopo kwa Chuo Kikuu Mzumbe kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara;

(iii) imefanikisha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule zifuatazo; Shule ya Msingi Kigongo - Misungwi, Shule ya Msingi Mugeza - Ngara, Shule ya

Msingi Sima A – Bariadi; Shule ya Msingi Ikungi - Singida Vijijini; Shule ya Msingi Mundindi – Ludewa na Shule za Sekondari za Wasichana za Rugambwa - Bukoba na Jangwani - Ilala;

(iv) imekamilisha kukarabati na kukabidhi shule 10 kongwe kati ya 17 za awamu ya kwanza. Shule hizo ni Shule za Sekondari Pugu, Mzumbe, Kilakala, Msalato, Ilboru, Same, Nganza, Mwenge, Tabora Wavulana na Tabora Wasichana;

(v) imeendelea na ukarabati wa Shule 7 za Sekondari ambazo ni Ruvu, Dodoma, Bihawana, Bwiru Wasichana, Sengerema, Kondoa Wasichana na Korogwe Wasichana;

(vi) imeendelea na ujenzi wa mabweni katika Shule za Sekondari Mkula - Busega, Kamagi - Sikonge, Inyonga - Mlele, Lulumba - Iramba, Kibakwe - Mpwapwa, Endasak - Hanang, Kilumba - Nyasa, Kisange - Kasulu, Muyenzi - Ngara, Kibaigwa - Kongwa na Ufana - Babati ambapo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Aidha, Ujenzi wa bweni katika Shule ya Msingi Munguli - Singida upo katika hatua za mwanzo;

(vii) imeandaa miongozo itakayotumika katika kazi za ufuatiliaji na tathmini ya miradi;

(viii) imeratibu ujenzi wa nyumba 40 za walimu ambapo nyumba 15 zimekamilika; na

(ix) imejenga matundu ya vyoo 312 na madarasa 39 katika shule 26.

**Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**32.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Mamlaka imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na kazi ya ujenzi wa chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Namtumbo ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018. Ujenzi wa chuo utakapokamilika utaongeza fursa ya mafunzo kwa vijana wapatao 600 katika fani mbalimbali za ufundi stadi;

(ii) imejenga jengo la karakana ya umeme wa viwandani katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa Mwanza ambapo ujenzi umefikia asilimia 90. Ujenzi utakapokamilika utaongeza fursa ya mafunzo kwa vijana katika fani ya umeme wa viwandani. Hatua hii itawezesha upatikanaji wa wataalamu wenye ujuzi

na umahiri wanaohitajika katika sekta mbalimbali za kujenga uchumi wa kati kupitia viwanda;

(iii) imekamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika mikoa ya Geita, Simiyu na Rukwa;

(iv) imeendelea na ujenzi wa Karakana ya Teknolojia ya Ushonaji katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Pwani. Ujenzi wa Karakana hiyo umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018;

(v) imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro na kwa sasa hatua ya majadiliano na mkandarasi inaendelea na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2018; na

(vi) imepata vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika fani ya umeme katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

**33. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Baraza limetekeleza yafuatayo:

(i) limekagua Vyuo 36 vya Elimu ya Ufundi sawa na asilimia 72 ya lengo na kuvisajili vyote baada ya kukidhi vigezo vya msingi vya kuanza mafunzo;

(ii) limeshauri na kuvielekeza Vyuo 26 vya Elimu ya Ufundi kuhusu utaratibu wa kufikia hatua ya Ithibati ambapo Vyuo 10 vimepata Ithibati ya Awali na Vyuo 16 vimepata Ithibati kamili;

(iii) limehakiki ubora wa mafunzo kwa Vyuo 460 vya Elimu ya Ufundi. Matokeo ya uhakiki yameonesha mapungufu kadhaa katika uendeshaji ukiwemo uwiano usioridhisha wa Mwalimu kwa Wanafunzi, uwepo wa Walimu wasio na sifa, uhaba wa miundombinu, mitaala ambayo haina ithibati. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kusitisha na kupunguza udahili;

(iv) limetengeneza na kuboresha mifumo ya kielektroniki kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Mifumo hii ni pamoja na:

a) Mfumo wa Udahili na Uhakiki kwa wanafunzi wa Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Afya vya Serikali ili kupata takwimu sahihi na kwa wakati na kusaidia kufanya maamuzi sahihi katika mipango ya elimu;

b) Mfumo Unganishi (*Intergrated System*) baina ya mifumo ya Baraza na vyuo (mitihani, udahili na uhakiki wa udahili). Mfumo huu unarahisisha udahili vyuoni, uhakiki wa wanafunzi waliodahiliwa pia kupata takwimu mbalimbali kama vile matokeo ya mitihani kwa programu mbalimbali na idadi za wanafunzi wanaosoma Elimu ya Ufundi na takwimu za wahitimu wanaomaliza programu mbalimbali zinazotolewa na vyuo vya ufundi nchini;

c) Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Rasilimaliwatu katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi ambao unahusika katika kusajili na kutoa takwimu kuhusu Rasilimaliwatu vyuoni; na

d) Mfumo wa Kuchakata Matokeo ya Mitihani na Mfumo wa Kupokea na Kuchakata Maombi ya Hati za Matokeo. Mifumo hii itawezesha kuzalisha hati za matokeo kwa wahitimu wa Vyuo vya Afya, Mifugo na Ualimu.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**34. Mheshimiwa Spika,** Mojawapo ya jukumu la Wakala ni kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa walimu na viongozi wa elimu, ili kuimarisha uongozi, kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya uongozi na uendeshaji wa elimu. Katika mwaka 2017/18, Wakala umetekeleza yafuatayo:

(i) umedahili walimu 1,831 (wanaume ni 1,039 (57%) na wanawake ni 792 (43%)) kwenye kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na kozi ya Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule. Aidha, Wakala umedahili Walimu Wakuu 704 wanaume ni 518 (73%) na wanawake ni 186 (17%) kutoka mikoa ya Mbeya, Iringa na Songwe wanaochukua kozi ya Astashahada ya Uongozi, Usimamizi na Utawala katika Elimu;

(ii) umeendesha mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Shule kwa walimu 49 wa shule zisizo za Serikali zilizo chini ya usimamizi wa Jumuiya za Kiislamu Afrika ili kuimarisha usimamizi wa taaluma. Mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu katika maeneo ya Usimamizi na Utawala wa Shule; Ushauri na Unasihi; Utekelezaji wa Sera za Elimu; Udhibiti wa Majanga shuleni; Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi; Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Shule; Usimamizi wa Raslimali za Shule; Usimamizi na Utunzaji wa Kumbukumbu za Shule pamoja na Usimamizi na Tathmini ya Mtaala;

(iii) umefanya ukarabati wa mabweni 2 yenye uwezo wa kuchukua wanachuo 450 na kumbi 2 za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanachuo 150 kila mmoja;

(iv) umekamilisha michoro kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kampasi za Mbeya na Mwanza ambazo zitakuwa na uwezo wa kudahili wanachuo 700;

(v) umefanya maboresho ya Mtaala wa Stashahada ya Menejimenti na Utawala katika Elimu (DEMA); na

(vi) umeratibu uendeshaji wa mafunzo kwa

Walimu 1,568 wa Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi (MEMKWA) yenye lengo la kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

**Bodi ya Huduma za Maktaba**

**35. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Huduma za Maktaba ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba kwa watu wote nchini; kuanzisha, kuendesha, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi ya Mikoa, Wilaya hadi Vijiji pamoja na kutoa mafunzo na kuendesha Mitihani ya Taaluma na Ukutubi. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Bodi imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha upatikanaji wa vitabu 25,966, kati ya hivyo Vitabu 316 vilipatikana kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 1975 ambayo inamtaka kila mchapishaji wa vitabu na majarida nchini kuwasilisha katika Bodi nakala 2 ya kila chapisho, vitabu 829 vilinunuliwa na vitabu 24,821 vilipatikana kupitia msaada. Aidha, magazeti 9,829 na majarida 1,458 yalipatikana. Machapisho haya kwa ujumla wake yanaongeza fursa ya wananchi kupata elimu;

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba

kwenye jumla ya shule 18 (Shule za Msingi 2 na Sekondari 16) ili kujenga utamaduni wa kujisomea na kuongeza maarifa; na

(iii) imetoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi 826 katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo kwa mchanganuo ufuatao: Cheti cha Msingi (NTA 4) wanafunzi **212**, Cheti (NTA 5) wanafunzi **287** na Stashahada (NTA 6) wanafunzi **327**.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**36.** **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo. Katika mwaka 2017/18 Bodi imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi **122,623** ambapo wanafunzi **33,244** ni wa mwaka wa kwanza na **89,379** ni wanaoendelea na masomo;

(ii) imetoa mikopo na ruzuku kwa jumla ya wanafunzi 351 wanaoendelea na masomo nje ya nchi: Urusi **16,** Ujerumani **22,** Ukraine mmoja**,** Misri **2,** Msumbiji **117,**

Algeria **168**, Cuba **24** na Serbia mmoja;

(iii) imeboresha mifumo ya uchambuzi, upangaji na urejeshwaji wa mikopo kwa kuunganisha mifumo hiyo na mifumo ya malipo ya kibenki na mfumo wa malipo wa Serikali;

(iv) imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 132.30 za mikopo iliyoiva sawa na asilimia 101% ya lengo la mwaka 2017/18, ambalo lilikuwa ni Shilingi bilioni 130;

(v) imeshiriki katika maonesho ya 12 ya Vyuo Vikuu na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) ambapo elimu juu ya shughuli za taasisi kwa wateja na wadau mbalimbali ilitolewa kwa wanafunzi na wadau wengine; na

(vi) imewabaini wadaiwa sugu 147,231 na kati yao 42,213 wameanza kufanya marejesho ya fedha za mikopo waliyopatiwa.

**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, kuhakiki ubora wa Elimu na kuidhinisha Programu zifundishwazo ili zikidhi mahitaji ya Taifa na soko la ajira. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Tume imetekeleza

yafuatayo:

(i) imeratibu zoezi la udahili ambapo jumla ya waombaji **63,737** (wanaume **38,779** na wanawake **24,958**) walidahiliwa katika vyuo mbalimbali. Aidha, Kati ya wadahiliwa hawa **50,292 (78.9%)** wamesajiliwa katika vyuo vya umma (wanaume **30,801** na wanawake **19,491**) na wadahiliwa **13,445 (21.1%)** wamesajiliwa katika Vyuo visivyo vya Serikali (Wanaume **7,978** na Wanawake **5,467)**;

(ii) imepokea maombi ya kutathmini na kuidhinisha programu **124** za masomo kutoka Vyuo Vikuu nchini. Jumla ya programu **21** zimepata idhini na programu za masomo **103** zinafanyiwa kazi na wataalam;

(iii) imepokea maombi ya kutathmini na kutambua tuzo **1,676** za ngazi mbalimbali zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchi za nje. Kati ya tuzo hizo **1,412** (87%) zilitambuliwa, tuzo **10** (0.59%) hazikutambuliwa na tuzo **254** (15%) ziliwasilishwa bila ya kuwa na taarifa zinazojitosheleza, hivyo waombaji wameelekezwa kuzikamilisha ili ziweze kufanyiwa tathmini; na

(iv) imeanza kutumia mfumo maalum wa *University Information Management System* (UIMS) kupokea taarifa mbalimbali ili kurahisisha utoaji wa taarifa za Vyuo Vikuu na kutengeneza kanzidata ikiwemo takwimu za wanafunzi waliodahiliwa, waliohitimu na taarifa za wahadhiri kwa ujumla wao.

**38. Mheshimiwa Spika,** ili kurahisisha utoaji wa taarifa za Vyuo Vikuu, Tume iliandaa maonesho ya 12 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Lengo la Maonesho hayo ilikuwa ni kutoa fursa kwa Vyuo kuonesha na kutangaza shughuli mbalimbali zinazoendeshwa na Chuo husika na kuwapa wanafunzi fursa ya kupata taarifa mbalimbali za vyuo.

**Tume ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**39. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Hati Idhini, Wizara ina wajibu wa kuimarisha utumiaji wa Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati pamoja na kuendeleza wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Katika mwaka 2017/18 Tume ya Sayansi na Teknolojia, imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imekamilisha vijarida vitatu vya taarifa ya kisera vinavyotoa ushahidi wa kisayansi (*Policy Briefs)* katika maeneo

yafuatayo:

(a) uzuiaji wa uharibifu wa mazao baada ya mavuno;

(b) upunguzaji wa migogoro ya wakulima na wafugaji; na

(c) uvunaji wa mazao ya baharini kwa upande wa Zanzibar.

(ii) imeandaa Kiunzi cha Kutathmini Maombi ya Uendelezaji wa Ubunifu uliotokana na matokeo ya utafiti uliofadhiliwa kwa kushirikiana na Serikali ya Afrika Kusini. Aidha, Kiunzi hiki kitatumika katika kutathmini maombi ya uendelezaji wa ubunifu nchini kwa kupitia fedha za kuendeleza Ubunifu katika Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE);

(iii) imefadhili miradi ya utafiti 20 inayoendelea ya utafiti inayofadhiliwa kwa kushirikiana na SIDA na imepokea mawazo ya miradi 387 katika maeneo ya viwanda, TEHAMA, kilimo, afya, mazingira na maliasili;

(iv) imeendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanga ambayo ipo kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji. Aidha, Tume

imetoa tangazo la kufadhili miradi mipya ya ukarabati wa miundombinu ya utafiti katika taasisi za utafiti na maendeleo; na

(v) imefadhili watafiti 27, (23 ni wa Shahada ya Uzamili na 4 Shahada ya Uzamivu) ambao wapo katika hatua mbalimbali za kuhitimisha masomo yao.

**Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania**

**40.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Tume ya Nguvu za Atomiki ya Tanzania imeendelea na jukumu lake la kudhibiti mionzi katika vituo vya huduma kwa kufanya yafuatayo:

(i) imepokea maombi 237 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ambapo maombi yote yalipata vibali baada ya kukidhi matakwa ya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya mwaka 2003. Vigezo vinahusisha chanzo cha mionzi, sifa za kitaaluma za msafirishaji na mtumiaji na mpango wa uhifadhi wa kudumu wa mabaki ya chanzo cha mionzi;

(ii) ilipima kiasi cha mionzi kwa wafanyakazi 423 kutoka katika vituo 68 kwa kutathmini kiasi cha mionzi kwenye vifaa vya kupima mionzi kwa wafanyakazi. Kiwango cha mionzi kwa wafanyakazi

kwa kipindi cha miezi mitatu kilikuwa chini ya 5 *microsivart,* kiwango ambacho kinakubalika kimataifa;

(iii) imekagua vituo 23 vinavyotumia mionzi na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama wa watumiaji na mazingira;

(iv) imesajili vituo vipya 56 vya watumiaji wa vyanzo vya mionzi na kufanya kuwa na jumla ya vituo 806 vinavyotumia mionzi;

(v) imetoa leseni 237 kwa wamiliki wa vyanzo vya mionzi;

(vi) imeendelea na ujenzi wa Maabara ya kisasa Awamu ya Kwanza ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2018; na

(vii) imepokea vifaa vya Maabara kutoka Jumuiya ya Umoja wa Ulaya. Vifaa hivyo vinasaidia kujenga uwezo wa Tume kutimiza majukumu yake katika usimamizi na uthibiti wa matumizi salama ya vyanzo vya mionzi.

**41. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya mionzi vinadhibitiwa na haviathiri mazingira na afya za viumbe hai, Wizara kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki:

(i) imekagua vituo vya mionzi katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mtwara pamoja na Mipaka ya Namanga, Tarakea, Sirari, Holili, Horohoro na Tunduma ili kutathmini hali ya vifaa vinavyotumika;

(ii) imefanya tathmini ya mahitaji kwa ajili ya kuboresha ulinzi na usalama wa vyanzo vya mionzi katika Kituo cha Matibabu ya Saratani cha Bugando;

(iii) imekagua na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama kwa watumiaji wa Vituo vitano vya *Ocean Road Cancer Institute (*Dar es Salaam), *Bugando Medical Centre* (Mwanza), *Vector and Vector Borne Diseases Research Institute* (Tanga), *Secondary Standard Dosimetry Laboratory* (Arusha) na *Central Radioactive Waste Management Facility* (Arusha). Vile vile, Wizara kupitia Tume imefungua ofisi zake katika mipaka ya Rusumo, Mtukula, Tarakea, Holili, Horohoro, Bandari ya Tanga na Tunduma kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mionzi ili kuzuia vyakula visiingie nchini kama havifai kwa matumizi ya binadamu;

(iv) imefanya upimaji wa viwango vya mionzi kwa sampuli 2,012 ili kuhakikisha

afya za wananchi zinalindwa dhidi ya mionzi. Kati ya sampuli hizi, 1,002 ni za vyakula vinavyoingia nchini, 602 ni za vyakula vinavyokwenda nje ya nchi, 112 ni za mbolea, 238 ni za vyakula vya wanyama na 58 ni sigara za aina ya Pall Mall (8), Winsten (12) na Marlboro (38);

(v) imetengeneza vifaa 43 vya elektroniki na vifaa 9 vya ukaguzi na uhakiki wa vifaa vya ujenzi wa barabara (*Troxler Gauges*) pamoja na mashine ya uhakiki wa mionzi (*Calibration Irradiation Machine*) katika Maabara ya Uhakiki wa Mionzi ya *Secondary Standard Dosimetry Laboratory* (SSDL);

(vi) imesimika mifumo na vifaa vya maabara na kutoa mafunzo ya namna ya kuvitumia pamoja na kuvifanyia matengenezo kwa lengo la kuboresha maabara ya *X- Ray Florescence* (*XRF), Gamma* na *Alpha;* na

(vii) imetoa mafunzo ya mifumo ya ubora kwenye maabara za kinyuklia kwa watumishi watatu wa Tume, yaliyoshirikisha washiriki 32 kutoka nchi 26 za Kanda ya Afrika.

**Vyuo vya Elimu ya Juu**

**42. Mheshimiwa Spika,** Elimu ya Juu ni mojawapo ya nguzo muhimu ya kuwezesha Serikali kufikia malengo yake ya maendeleo kwa kuzalisha rasilimaliwatu yenye ujuzi stahiki. Hivyo, Wizara imeendelea kuratibu shughuli zake ikiwa ni pamoja kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuinua ubora na kuongeza fursa kwa wanafunzi wengi zaidi kujiunga na Elimu ya Juu. Katika mwaka 2017/18, Vyuo Vikuu vimetekeleza yafuatayo:

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**43. Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Huria kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimetoa mafunzo ya ana kwa ana ya Shahada ya Uzamili katika Programu za *Masters of Community Economic Development* (MCED) na *Masters of Arts in Social Work* (MASW) kwa kutumia mfumo wa *Blended Learning Mode (Learning Management System and Face to Face)*;

(ii) kimetekeleza mpango wa Serikali wa kuunganisha mifumo yake ya kieletroniki kama vile *Student Academic Registration Information System* na kuwezesha malipo

ya ada kufanyika moja kwa moja kieletroniki katika mfumo wa Serikali wa *Government e-Pay Gateway* kupitia Wizara ya Fedha na Mipango; na

(iii) kuendelea kutoa bila gharama yoyote mafunzo ya TEHAMA kwa wanafunzi wenye ulemavu, ambapo wanafunzi wasioona 42 na viziwi 37 walipatiwa mafunzo.

**Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**44. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kimefanya yafuatayo:

(i) kimetekeleza mradi wa *Council for the Development of Social Science Research in Africa (CODESRIA)* kuhusu mitaala ya Vyuo Vikuu na mahitaji ya soko;

(ii) kimeratibu uwasilishaji wa matokeo ya tafiti kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu 10 na kwa wanafunzi wa Shahada za Uzamili 115;

(iii) kimekamilisha uchapaji wa kitabu cha majumuisho ya warsha za utafiti kuhusu Maendeleo ya Ushirika;

(iv) kimeendelea kuratibu zoezi la kutoa machapisho matatu ambayo ni (*Jounal of*

*Cooperative and Business Studies, Research Report Series Journal na Workshop Proceeding on "The Joint Workshop on Innovation and Enterpreneurship in Cooperative, The Private Sector and Public Services; Lesson From Sweden and Tanzania)*; na

(v) kimeboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kufanya ukarabati wa nyumba 6 za makazi, mabweni 16 na majengo 2 ya ofisi na kubadili matumizi ya jengo moja na kuwezesha kupatikana kwa ofisi 5 za watumishi kupitia mradi wa *Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support" (MIVARF)*.

**Chuo Kikuu cha Ardhi**

**45.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimetoa huduma za ushauri kwa jamii na kutekeleza miradi mbalimbali ya ushauri wa kitaaluma ikiwa ni pamoja na *Master Plans* za miji ya Geita, Kilwa, Nzega, Urambo, Sikonge na Mafinga;

(ii) kimefanya miradi ya utafiti 69 kati ya miradi 30 iliyotarajiwa kufanyika kwa mwaka 2017/18. Baadhi ya Miradi hiyo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti na uvumbuzi kwa

ajili ya kutunza ardhi na usimamizi wa mazingira kwa maendeleo ya nchi na kuwajengea wananchi uwezo wa kupunguza maafa hasa kwa wanajamii wanaoishi maeneo hatarishi Tanzania (*Regional Disaster, Risk and Vulnerability Reduction Capacity Development);*

(iii) kimegharamia mafunzo kwa Watumishi waendeshaji 25 wa Shahada ya Uzamili, 12 wa Shahada ya Kwanza, 20 wa Stashahada. Aidha, kimegharamia mafunzo kwa wanataaluma 56 wa Shahada ya Uzamivu na 22 wa Shahada ya Uzamili; na

(iv) kimefanya ukarabati wa mabweni 5 na kuwezesha wanafunzi 457 kupata malazi katika chuo hicho.

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**46. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2017/18 Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeongeza idadi ya miradi ya utafiti kutoka 145 hadi 209; machapisho yameongezeka kutoka 337 hadi 354 na majarida kutoka 21 hadi 46. Tafiti hizo, zililenga kuboresha Teknolojia ya Kuzalisha Togwa ya Ndizi, Kukuza Sekta ya Mafuta na Gesi, Kuboresha na

Kuhifadhi Mazingira na Kutengeneza Teknolojia rahisi ya kutenganisha Madini ya Shaba ili kuwawezesha Mafundi Mchundo na Wachimbaji wadogo wadogo kutenganisha shaba kwa ufanisi na tija;

(ii) kinaendelea kukamilisha ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua katika mabweni mapya ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 60. Ujenzi utakapokamilika utasaidia kuondoa maji ya mvua yanayosimama katika eneo hilo; na

(iii) kimeendelea na ukamilishaji wa kazi za nje za ujenzi wa jengo la maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,600, ukumbi wa mkutano wenye uwezo wa kuchukua washiriki 600 na *Conficius Institute* yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja.

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**47.** **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimegharamia masomo kwa jumla ya wafanyakazi 377; katika nyanja za Shahada ya Uzamivu (220), Shahada ya

Uzamili (113), Shahada ya Kwanza (20), Stashahada na Astashahada (24);

(ii) kimefanya utafiti wa nishati Mbadala za Kupikia Katika Kaya nchini Tanzania, lengo ni uboreshaji wa makaa ya mawe na mabaki ya kilimo (*bio - briquettes)* kwa ajili ya matumizi ya kupikia kwenye kaya;

(iii) kimefanya utafiti katika Kanda ya Kati wa Kutambua *Sumu Kuvu* (*Aflatoxins*) katika vyakula vilivyo tayari kupikwa miongoni mwa kaya na uelewa wa jamii juu ya Sumu Kuvu kwenye vyakula vya watoto;

(iv) kimeratibu tafiti 4 zilizolenga kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu chini ya mradi wa LANES katika maeneo yafuatayo:

(a) Kiunzi cha Upimaji wa Stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu kwa Watoto (*National Framework for the Assessment of Children's Literacy and Numeracy Learning in Tanzania*);

(b) Mazingira ya nyumbani na darasani yanavyochangia katika kujenga Stadi za Kusoma na Kuhesabu kwa wanafunzi wa Darasa la I & II (*Promoting Reading and Arithmetic*

*Skills Among STD I & II Pupils in Tanzania Primary Schools; The Role of Home and Classroom Environment*);

(c) Kukuza Ufahamu kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi kwa kupitia Maudhui ya Kielektroniki (*Enhancing Early Grade Primary School, Pupils' Comprehension Through E-Content*); na

(d) Kukuza Umahiri wa Usomaji wa Watoto kwa kupitia Mkakati wa Kumuendeleza Mwalimu (*Improving Pupils' Reading Fluency Ability in Early Grade Through Teacher Development Strategy in Five Selected Districts).*

Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia wadau wote wa elimu kupata ufumbuzi wa changamoto za ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Msingi. Aidha, wadau wa elimu wataelewa umuhimu wa kufundisha na kujifunza kwa kutumia maudhui ya kielektroniki na kuweka mikakati ya jinsi ya kuitumia.

**Chuo Kikuu cha Mzumbe**

**48. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimehuisha mitaala ya Programu 2 kati ya 11 za Shahada *(MSc Environment Management na MA Development Policy)* ili kuendana na Mwongozo wa Vyuo Vikuu wa mwaka 2006;

(ii) kimejenga madarasa na jengo la utawala Kampasi ya Mbeya ili kuongeza majengo ya ofisi, na hivyo kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za utawala chuoni; na

(iii) kimetekeleza mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango wa kuunganisha mifumo yake ya kieletroniki kama vile *Student Academic Registration Information System* na kuwezesha malipo ya ada kufanyika moja kwa moja kieletroniki kupitia mfumo wa Serikali wa *Government e-Pay Gateway.*

**Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**49. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimefanya utafiti wa Genetiki na Uzalishaji wa mbegu bora za mazao ambao umewezesha chuo kuzalisha mbegu bora nne za maharage kama zifutavyo: SUA 90-1990; Rojo-1997; Mshindi-2006; na Pesa-2006. Sifa za mbegu hizi ni kuzaa zaidi na kustahimili

ukame na magonjwa. Aidha, maharage yake huiva kwa haraka yanapopikwa ukilinganisha na mbegu za asili. Mbegu hizi zimeanza kuzalishwa na wakulima katika baadhi ya sehemu za Mikoa ya Morogoro na Kilimanjaro. Pia mbegu hizi bora zimetumiwa na wazalishaji wa mbegu kuzalisha mbegu bora zaidi hapa nchini na katika nchi tunazoshirikiana nazo ambazo ni Marekani na Zambia;

(ii) kimefanya utafiti kuhusu Sayansi na Teknolojia ya Chakula ambapo utafiti huo umegundua matumizi ya unga wa ubuyu kwa matumizi mbalimbali hususan katika kutengeneza "jam" na kujiongezea kipato. Matokeo ya utafiti huu yamepata haki miliki yenye namba TZ/P/10/CC276 kutoka (*Business Registrations and Lincensing Agency - BRELA*) ya mwaka 2016;

(iii) kimefanya utafiti kuhusu kuzalisha Mbegu bora mbili za mpunga ambazo ni Mwangaza na Kalalu. Mbegu hizi zimesaidia wakulima wa zao la mpunga kukabiliana na ugonjwa wa mpunga ujulikanao kama "*Rice Mottle Virus*" na hivyo kuwa na kilimo cha mpunga chenye tija. Mbegu hizi zinakomaa mapema na hazishambuliwi na wadudu tajwa;

(iv) kimefanya utafiti wa kutumia menejimenti ya ekolojia kudhibiti panya kwenye mazao ya mahindi na mpunga. Mradi huu umebuni teknolojia ya kudhibiti panya waharibifu na hivyo kuongeza uzalishaji na pato la wakulima;

(v) kimefanya utafiti kuhusu magonjwa ambukizi ya binadamu na mifugo. Utafiti huu umeboresha ukusanyaji wa taarifa za magonjwa kwa haraka na utengenezaji wa zana za utambuzi wa magonjwa vijijini hasa ya mlipuko na hivyo kupunguza athari za magonjwa hayo kwa jamii kupitia *African Centre of Excellence for Infectious Diseases;*

(vi) kimeandaa mitaala mipya 10 ya Shahada ya Kwanza na 7 ya Shahada za Uzamili;

(vii) kimenunua jumla ya vitabu 1,018 katika fani 594 kati ya vitabu 1,000 vilivyopangwa kununuliwa; na

(viii) kimeanza ujenzi wa jengo la wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu katika Shule Kuu ya Uchumi Kilimo na Masomo ya Biashara.

**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**50. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2017/18 chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeendelea na tafiti mbalimbali zikiwemo tafiti za magonjwa yasiyoambukiza, yanayoambukiza na yasiyopewa kipaumbele kama vile Tafiti za Ukimwi *(DNA-prime HIV vaccine, Key population size estimation and intergrated Biobehavioral surveys*), malaria (*Atemethanine resistance studies*), Kichocho *(Female Genital Schistosomiasis and Linkage to HIV)* na magojwa yasiyoambukiza (*Etiology of esophagial cancer, genetics of cancer, Gene-expert for Diagnosis of Breast Cancer);*

(ii) kimeendelea kutoa huduma na mafunzo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Mifupa Muhimbili;

(iii) kimeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na Afya ya Binadamu kwa serikali kama vile Mpango wa kuzuia Malaria, UKIMWI, Chanjo kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama UNAIDS, UNICEF na WHO;

(iv) kimeboresha jukwaa la kujifunzia kupitia TEHAMA (*E-learning platform)* kwa wanafunzi wa Shahada mbalimbali ikiwemo Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii - *Masters of Public Health* kwa masafa yanatumia jukwaa hili;

(v) kimeendelea na ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo Kampasi ya Mloganzila;

(vi) kimekamilisha Mwongozo wa Tiba na Njia Bora za Kujikinga na VVU ili kuwezesha watoa huduma kutoa huduma kwa usahihi na kwa umahiri;

(vii) kimeratibu ufunguzi wa majaribio (*mock opening*) na ufunguzi laini (*soft opening*) wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Mloganzila ili kuanza kutoa huduma za tiba katika hospitali hiyo; na

(viii) kimeendelea na ujenzi wa mabweni na majengo mengine ya ufundishaji kwenye Kampasi ya Mloganzila.

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**51.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/18 Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeendelea na jumla ya miradi 5 ya shughuli za utafiti na kutoa machapisho 6;

(ii) kimeanzisha programu za Shahada ya Uzamili katika Elimu kwa masomo ya Kemia, Baiolojia na Jiografia;

(iii) kimewezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanafunzi na wanajumuiya ya chuo kwa kufanikisha ujenzi wa jengo la huduma za kibenki kwa ushirikiano na Benki ya CRDB;

(iv) kimewajengea uwezo wafanyakazi 78 katika ngazi mbalimbali ambapo wanataaluma 67 na wafanyakazi waendeshaji 11 wako masomoni; na

(v) kimeboresha na kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kumalizia ujenzi wa ukumbi wa mihadhara ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1200 kwa wakati mmoja na utakuwa na vyumba 20 vya ofisi za Walimu na vyumba 2 vya kuhifadhi mitihani.

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**52. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi 47 wenye mahitaji maalum;

(ii) kimeimarisha miundombinu ya TEHAMA kwa kununua vifaa vya Mfumo wa Mtandao wa Taarifa za Kijiografia ikiwemo ununuzi na uunganishaji wa Kompyuta 20; Aidha kimenunua Kompyuta 10 kwa ajili ya maabara ya wanafunzi na 25 kwa ajili ya wafanyakazi;

(iii) kimeajiri wafanyakazi 16 kati yao 10 wanataaluma na 6 waendeshaji; na

(iv) kimeajiri wafanyakazi 16 kati yao 10 wanataaluma na 6 waendeshaji.

**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**53. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimenunua na kufunga vifaa vya kisasa vya kufundishia na kufunga viti visivyohamishika kwenye madarasa 5 katika Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 692 kwa wakati mmoja. Vifaa na viti hivyo vimeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(ii) kimekamilisha ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi katika Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 720 kwa wakati mmoja. Kukamilika kwa Hosteli hii kumeongeza fursa ya wanafunzi kuishi katika mazingira bora na tulivu; na

(iii) kimepata vitabu 20,000 vipya kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya maktaba ya Chuo, uwepo wa vitabu hivyo umeboresha huduma za maktaba.

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**54. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeandaa mitaala 12 na kuwasilishwa Tume ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya kupatiwa ithibati. Mtaala wa Stashahada ya Uhandisi wa Vifaa Tiba umepata ithibati sambamba na Idara itakayokuwa na dhamana ya kutoa mafunzo hayo;

(ii) kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 105, Stashahada mmoja, Shahada ya Kwanza 20, Shahada ya Uzamili 52 na Shahada ya Uzamivu 32. Aidha, watumishi 41 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi;

(iii) kimetoa ushauri elekezi katika miradi ifuatayo:

(a) ukarabati wa shule za sekondari 17 na vyuo vya ualimu 15 vya Serikali;

(b) ujenzi wa ofisi za Halmashauri za Wilaya za Kiteto na Mafia;

(c) kiwanda cha kusaga nafaka cha *East African Starch Ltd* kilichopo Mbeya;

(d) barabara ya lami Sumbawanga; na

(e) jengo la *X-ray* katika Hospitali ya Kanda ya Rufaa Mbeya.

(iv) kimeendelea na ujenzi wa maktaba awamu ya kwanza ambao umekamilika kwa asilimia 57. Jengo hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2500 kwa wakati mmoja.

**Chuo cha Ufundi Arusha**

**55. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimedahili wanafunzi **900** wa mwaka wa kwanza (Astashahada na Stashahada);

(ii) kimeanzisha programu tatu **(3)** mpya ambazo ni *"Pipe Works, Oil and Gas Engineering"* (Astashahada), *"Electrical and Hydropower Engineering"* (Astashahada) na *"Electrical & Automation Engineering"* (Shahada);

(iii) kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa jumla ya watumishi 43 na watumishi 11 waligharamiwa mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo haya yataongeza umahiri wa watumishi katika kutoa mafunzo, kufanya tafiti pamoja na ushauri wa kitaalamu ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia;

(iv) kimepata vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia iliyonunuliwa kwa mkopo nafuu kutoka Serikali ya Austria kwa ajili ya Karakana 2 za Uhandisi Magari na Karakana 1 ya Useremala. Vifaa hivi vitasaidia kuongeza wataalamu wa ufundi (nguvu kazi) kwenye sekta ya viwanda ili kutekeleza Sera ya nchi kuelekea kwenye Uchumi wa kati wa viwanda; na

(v) kimekamilisha ujenzi wa bwawa la kuvuna maji ya mvua, mifereji ya umwagiliaji na miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mafunzo ya umwagiliaji Oljoro.

**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**56. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 2,089 (wanaume 1,648; wanawake 441) ambapo, Stashahada ya Kawaida ni 1,063; Shahada ya Kwanza ni 998 na Shahada ya Umahiri ni 28. Aidha, imesajili wanafunzi 17 katika Kampasi yake mpya ya Myunga iliyopo Songwe kwa ajili ya kozi mpya ya Ufundi Mchundo katika Teknolojia ya Habari (*Technician Certificate NVA Level 3 Technician Certificate NVA Level 3*);

(ii) imeandaa Mtaala na kuanzisha kozi mpya ya Stashahada ya Kawaida ya Teknolojia ya Bidhaa za Ngozi (*Ordinary Diploma in Leather Products Technology (NTA Level 4-6*) katika Kampasi ya Mwanza na kuuwasilisha kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) kwa ajili ya kupatiwa ithibati. Vilevile imeandaa mtaala wa kuanzisha kozi mpya ya Shahada ya Umahiri katika Uhandisi wa Nishati Endelevu (*Masters of Engineering in Sustainable Energy*) na kupata ithibati ya NACTE. Masomo yataanza mwaka wa masomo wa 2018/19;

(iii) imenunua magari 2 (Basi aina ya Isuzu yenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 60 na *Toyota Hilux Double Cabin)* kwa ajili ya kuwezesha mafunzo viwandani;

(iv) imegharamia chakula kwa wanafunzi 683 na mafunzo kwa vitendo (*Industrial Practical Training)* kwa wanafunzi 550 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT); na

(v) imeweka vifaa vya TEHAMA katika jengo la kufundishia (*Teaching Tower*) na samani katika baadhi ya vyumba.

**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha**

**57. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili wanafunzi 187 na kufikisha jumla ya wanafunzi 400 kutoka 213 ikiwa ni ongezeko la asilimia 88. Ongezeko hili limetokana na msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na Vituo Mahiri katika kufadhili wanafunzi;

(ii) imeandaa program 2 za uzamili na uzamivu ambazo ni PhD in *Innovation and Management* na *MBA in Intelectual*

*Property Right* na kuwasilishwa TCU kwa ajili ya kupewa ithibati. Aidha, imeandaa mitaala 10 katika Shule ya Sayansi ya Viumbe Hai na Uhandisi Biolojia (*Life Sciences and Bio- Engineering*) na Sayansi ya Hisabati na Ukokotoaji;

(iii) imefungua vituo vinne vya Umahiri vya kimataifa vinavyofadhiliwa na wafadhili mbalimbali. Vituo hivi ni:

(a) kituo cha Utafiti na Umahiri katika Ufundishaji Endelevu katika Chakula na Uhifadhi wa Virutubisho na usalama wa chakula - *Centre for Research, Agricultural advancement, Teaching Excellence and sustainability in food and nutritional security* kinachofadhiliwa na Benki ya Dunia;

(b) kituo cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu - *Water Infrusructure and Sustainable Energy* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia;

(c) kituo cha TEHAMA Afrika Mashariki - *Centre of ICT in East Africa* kwa ufadhili wa DAAD Ujerumani; na

(d) kituo cha Ubunifu wa Teknolojia na Nishati (*Innovative Technology*

*and Energy)* chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea.

(iv) inatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya majitaka ya machinjio ya Mwanza kwa kujenga mfumo wa kisasa wa kusafisha majitaka yatokanayo na machinjio kuu na kuzalisha gesi kwa matumizi ya machinjioni. Mradi huu uko katika hatua za majaribio ya mwisho; na

(v) imeanzisha mradi wa utafiti wa uzalishaji wa ndizi bora na zenye kuhimili magonjwa ambapo imeanzisha vituo vya mafunzo Tarakea na Lyamungo kwa ajili ya kutoa mbegu bora za migomba ya aina mbalimbali.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18

### Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu - EP4R)

**58.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga katika kuimarisha Sekta ya Elimu kwa kuzingatia ubora na usimamizi wa rasilimali fedha na manunuzi ya umma kwa ajili ya mipango ya elimu. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara

kupitia mradi wa Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imeandaa michoro ya majengo, makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi 50 za Uthibiti Ubora wa Shule. Kazi inayoendelea ni kuchambua gharama za ujenzi kutoka kwa wakandarasi. Kazi ya ujenzi itaanza mwezi Juni, 2018;

(ii) imewezesha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Vyuo 7 vya Ualimu Awamu ya Pili ambapo ukarabati upo katika hatua mbalimbali. Vyuo hivyo ni Tandala, Nachingwea, Tarime, Kinampanda, Mandaka, Patandi na Ilonga Aidha, Chuo cha Murutunguru kimeanza kujengwa upya kufuatia taarifa ya Wahandisi kubaini kuwa chuo hicho kimechakaa na hakifai kufanyiwa ukarabati;

(iii) imegharamia ujenzi wa mgahawa wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja katika Bweni la Nicholous Kuhanga Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambapo ujenzi umefikia asilimia 70 ya ukamilishaji;

(iv) imenunua magari 54 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora wa shule na ufuatiliaji na tathmini;

(v) imewezesha kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa utakaokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa mkupuo;

(vi) imewezesha ujenzi wa maabara katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa – MUCE kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa walimu wa masomo ya Sayansi katika shule za sekondari;

(vii) imesimamia na kutekeleza vipaumbele na viashiria vya Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo *(Education Program for Results - EP4R*) na kuwezesha Serikali kupata Dola za Kimarekani milioni 49.7 sawa na **Shilingi 109,340,000,000.00;** na

(viii) imewezesha ujenzi wa miundombinu katika Shule 290 (Msingi 180 na Sekondari 110) ikiwemo madarasa 1,308, matundu ya vyoo 1,560, mabweni 129, nyumba za walimu 8 (*2 in one*), mabwalo 7, majengo ya utawala 10, maabara 4 na maktaba 1.

### Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya KKK

**59.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wenye umri wa miaka 5-13 walio ndani na nje ya mfumo rasmi. Mpango huu unafadhiliwa na mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu *(Global Partnership for Education-GPE Fund).* Katika mwaka 2017/18 Wizara kupitia mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya KKK *(GPE-LANES)* imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

(i) ukamilishaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule ambacho kimepitishwa na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na kitawezesha kufanya shughuli za uthibiti wa ubora wa shule kwa ufanisi zaidi;

(ii) ununuzi wa pikipiki 2,894 ambazo zitasambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali katika mikoa 19 ifikapo mwezi Juni, 2018;

(iii) imenunua magari 5 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora wa shule; na

(iv) kuandaa maudhui ya kieletroniki na kuweka mikakati ya kutumia maudhui

hayo katika ufundishaji na ujifunzaji wa KKK. Rasimu ya awali imekamilika na iko katika kufanyiwa majaribio.

**Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**60. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umejikita katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vya Ualimu pamoja na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia mradi huu imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

(i) umegharamia ununuzi wa vitabu 1,948 vya fani za umeme, madini, ujenzi na umwagiliaji katika;

(ii) umegharamia usanifu wa jengo la ghorofa tatu la maabara, madarasa na ofisi za wakufunzi katika Chuo cha Ufundi Arusha. Mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo amekabidhiwa eneo la ujenzi tarehe 19 Machi 2018 na kazi ya ujenzi inaendelea; na

(iii) umegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi saba wa Chuo cha Ufundi Arusha na watumishi watano wa Vyuo vya Ufundi Stadi.

**Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu**

**61.** **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Canada. Mradi unalenga kuboresha miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzi katika vyuo vinne vya ualimu. Katika mwaka 2017/18 Wizara kupitia mradi huu imetekeleza shughuli zifuatazo katika Vyuo vya Ualimu vya Ndala, Shinyanga, Kitangali na Mpuguso:

(i) imekamilisha ujenzi wa jengo la nyumba za walimu la ghorofa 2 kwa ajili ya familia 4 ambalo tayari limekabidhiwa katika Chuo cha Ualimu Shinyanga. Aidha, imeendelea na ujenzi wa majengo 2 ya bweni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 152 kila moja na ujenzi wa uzio kwa ujumla umekamilika kwa asilimia 90. Aidha, Ujenzi wa majengo 2 ya madarasa yenye vyumba 8, ujenzi wa maktaba na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara vimefikia asilimia 60;

(ii) imeendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu Mpuguso yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 308, nyumba za walimu majengo 3 ya ghorofa na nyumba 1 ya kawaida kwa ajili ya familia 13 vyote kwa ujumla vimekamilika kwa asilimia 85. Ujenzi

wa maktaba, maabara, ukumbi wa mihadhara, ukumbi wa mkutano na ujenzi wa vyoo ambavyo kwa ujumla vimekamilika kwa asilimia 62;

(iii) imeendelea na ujenzi wa nyumba 11 za Wakufunzi katika Chuo cha Ualimu Kitangali ikiwemo nyumba ya Mkuu wa Chuo ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 68. Aidha, ujenzi wa madarasa vyumba 16, maktaba, ukumbi wa mihadhara kwa wanafunzi 240, na majengo mawili ya mabweni yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 308 umefikia asilimia 60; na

(iv) imeendelea na ujenzi wa nyumba 5 za wakufunzi (ikiwemo nyumba ya Mkuu wa Chuo) katika Chuo cha Ualimu Ndala; majengo 2 ya ghorofa kwa ajili ya wakufunzi yenye uwezo wa kuchukua familia 8; vyote kwa ujumla vimekamilika kwa asilimia 70. Aidha, katika sehemu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Ualimu Ndala, Mkandarasi Skywards Construction company alikabidhiwa eneo la ujenzi tarehe 27.11.2017. Ujenzi katika sehemu hii unahusisha: mabweni 2 ya ghorofa, madarasa ghorofa 2, jengo la mihadhara, maktaba na maabara. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 24.02.2018 na inatarajiwa kukamilika kwa kipindi cha miezi 18

tangu kuanza kwa kazi. Kwa sasa ujenzi upo hatua ya msingi kwa majengo yote.

**Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu**

62. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unalenga kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu katika Vyuo 35 vya Ualimu vya Serikali. Katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia mradi huu imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Vyuo 35 vya Ualimu ili kuweka mazingira rafiki ya utoaji elimu ya Ualimu;

(ii) imeanza Mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Ualimu ili kuwa na mtaala unaokidhi mahitaji ya sasa na unaoendana na mtaala wa elimu msingi ulioboreshwa;

(iii) imetangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa na Kemikali za Maabara za Sayansi kwa Masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia kwa ajili ya vyuo vya ualimu kuwezesha ujifunzaji wa masomo hayo kwa vitendo;

(iv) imetangaza zabuni ya Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji;

(v) imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 120 yaliyojumuisha elimu ya jinsia na elimu jumuishi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika Vyuo vya Ualimu; na

(vi) imempata mkandarasi na mshauri elekezi wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ili kuongeza uwezo wa kudahili na pia kuweka mazingira mazuri ya ujifunzaji kwa kuwa majengo yaliyopo hayafai kwa ukarabati. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei 2018.

**TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**63. Mheshimiwa Spika**, Baada ya kueleza mafanikio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) kwa mwaka 2017/18 naomba sasa nitoe utekelezaji wa Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18).

**64. Mheshimiwa Spika,** Tume hii ina jukumu la kuratibu na kutoa ushauri kuhusu Elimu, Sayansi, Habari na Utamaduni katika muktadha wa kimataifa. Aidha, Tume inashiriki katika kutengeneza viwango vya ubora vinavyotakiwa katika Nyanja ya Elimu, Sayansi na Utamaduni kwa kutoa maoni moja kwa moja au kwa kushirikisha wadau kutoa maoni katika maandalizi ya nyaraka mbalimbali kama vile mikataba na makubaliano ya kimataifa.

**65. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Tume ilikadiria kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 40,000,000.00.** Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Tume imekusanya jumla ya **Shilingi 57,529,487.17** sawa na asilimia **144** ya lengo.

**66. Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2017/18 yalikuwa ni **Shilingi 663,123,000**.00 (Mishahara **Shilingi 330,830,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 332,293,000**). Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2018 Tume imepokea jumla ya **Shilingi 500,972,100** sawa na asilimia **76** ya makadirio. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 246,668,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 254,304,100.00.**

**67. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2018 Tume imetumia jumla ya **Shilingi 425,223,615.00** sawa na asilimia **85** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 246,668,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 178,555,615.00.**

**68. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18 Tume imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeratibu udhamini kwa ufadhili wa UNESCO wa mafunzo kwa watanzania 8; nchini Korea 3, Ireland 1, Israel 1 na China 3;

(ii) imeandaa, kuchapisha na kusambaza jarida la “Tanzania na UNESCO” Toleo la 14 ambapo nakala 700 zimesambazwa kwa wadau mbalimbali;

(iii) imeandaa maandiko 7 ya Miradi ya kuboresha Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Mawasiliano na Habari pamoja na Utamaduni na Urithi wa Dunia kwa ajili ya ufadhili kutoka UNESCO na Wadau wengine;

(iv) imetoa mafunzo ya namna ya kutambua, kuhakiki ubora wa taarifa kwa wanafunzi wa Sekondari za Jangwani, Azania, Tambaza na Zanaki;

(v) imekagua na kufanya tathmini katika Hifadhi ya Milima ya Udzungwa ili kuona kama kuna uwezekano wa kuwa na maeneo Tengefu ya Ndege;

(vi) imekagua Mradi wa *“Heritage Archive of Tanzania”;*

(vii) imetoa mafunzo kwa wanachuo na vijana mbalimbali kuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia yaliyofanyika Zanzibar;

(viii) imekusanya data ili kusaidia katika program ya *Preservation of Digital Heritage (Collection of Arabic Manuscripts and Books);*

(ix) imeratibu Ushiriki wa nchi yetu pamoja na ripoti za Mtandao wa Kishule wa UNESCO-ASP Net, nchini Kenya; na

(x) imeshiriki katika mikutano mikuu iliyofanyika nchini Ghana, Ufaransa na Ujerumani kuhusu maeneo Tengefu *(Biosphere Reserves)* iliyojadili juu ya Kupunguza Umaskini Kupitia Maendeleo Endelevu.

**69. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza kwa kirefu utekelezaji wa mafungu yote mawili yaani Fungu 46 na Fungu 18 naomba sasa nielezee Mpango na Bajeti ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2018/19.

## C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA 2018/19

**70. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara yangu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

### Kuendeleza Elimu ya Msingi kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu

**71. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Vyuo vya Elimu ya Ualimu vitadahili jumla ya wanachuo **8,152** wa Mafunzo ya Ualimu wakiwemo **2,470** wa ngazi ya Astashahada na

**5,682** wa ngazi ya Stashahada ya masomo ya Sayansi (2,863), Elimu Maalum (395), Elimu ya Ufundi (116), Elimu ya Awali (1,563), Masomo ya Fani (124), Michezo (315), Elimu ya Msingi (762) na Stashahada ya Sayansi Jamii (2,014).

**72.** **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo, Wizara itatoa mafunzo kwa Wanachuo **20,535** wa Vyuo vya Ualimu wa mwaka wa Kwanza hadi wa Tatu ili kuoanisha nadharia na vitendo. Aidha, itatoa mafunzo kabilishi kwa Wanafunzi wasichana 200 wa Kidato cha Sita wa masomo ya Sayansi na Hisabati wenye sifa pungufu (*Principal Pass* moja na *Subsidiary* moja) kwenye masomo ya kufundishia ili wapate sifa stahiki za kusomea Stashahada ya Ualimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

**Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo Katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kuviimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kutoa mafunzo bora kwa kufanya yafuatayo:

(i) kujenga mazingira bora ya kutolea mafunzo kwa kujenga na kukarabati Miundombinu katika Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) kuwajengea uwezo Wakufunzi na Watumishi wengine 250 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili waweze kutoa elimu bora ya nadharia na vitendo kwa wanafunzi;

(iii) kuratibu zoezi la tathmini ya kubaini mahitaji ya sasa ili hatimaye kuandaa mitaala ya kozi fupi zitakazopewa ithibati na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi pamoja na kozi zitakazo lenga kuleta chachu ya maendeleo ya wananchi katika eneo husika; na

(iv) kugharamia chakula kwa wanafunzi 5,050 katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi.

**Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi**

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kusimamia Sera, Sheria na Miongozo katika Sekta ya Elimu ili kuhakikisha kuwa elimu katika ngazi zote inatolewa kwa ubora unaokusudiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itapitia Sera ya Elimu na Mafunzo kwa Lengo la kuhakikisha kuwa inaendana na hali halisi ya sasa;

(ii) itapitia Miongozo na Nyaraka mbalimbali zinazohusu utoaji wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari nchini ili ziendane na mahitaji ya sasa; na

(iii) itaandaa miongozo na nyaraka kadri mahitaji yatakavyojitokeza.

**Kuainisha Mahitaji ya Nchi Katika Ujuzi na Kuuendeleza**

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19, Wizara kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kazi kwa ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi itatekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za kazi kwa kutoa ruzuku kwa ushindani kwa Vyuo vya Ufundi nchini;

(ii) kuendelea kutoa ruzuku za Masomo ya Ufundi kupitia Skimu za Vocha za Mafunzo (*Trainee Voucher Scheme*) kwa vijana wasio na uwezo wa kujiendeleza ambapo jumla ya vijana 7000 watanufaika;

(iii) kuviwezesha Vyuo 20 vya Maendeleo Wananchi kutoa mafunzo ya ufundi kwa kuvikarabati na kuvinunulia vifaa;

(iv) kuzijengea uwezo taasisi za VETA, NACTE na TCU ili kusimamia Ubora wa

Elimu ya Ufundi na Stadi za Kazi; na

(v) kuimarisha Vyuo vya VETA na Elimu ya Ufundi kwa kuvinunulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya Uanagenzi (*Apprenticeship*).

**Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**76.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kusimamia Ithibati ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu na Kusimamia Ubora wa Elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kuanzisha mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vituo Nje ya Mfumo Rasmi;

(ii) kufanya ufuatiliaji wa Shule, Vyuo vya Ualimu na vituo Nje ya Mfumo Rasmi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kuangalia kama vinakidhi vigezo;

(iii) kukagua jumla ya asasi **11,327** zikiwemo shule za Msingi **8,785** za Sekondari **2,480** na Vyuo vya Ualimu **62**;

(iv) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Miongozo na Nyaraka kuhusu uboreshaji wa Elimumsingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu;

(v) itafanya tafiti mbalimbali za kielimu kwa lengo la kubaini changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji ili ziweze kupatiwa ufumbuzi; na

(vi) itakarabati Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule 40 za Wilaya za zamani kwa gharama ya **Shilingi Billioni 1.5**.

**Usimamizi wa Elimu ya Msingi na Sekondari**

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari, katika mwaka 2018/19 Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa Mwongozo wa Kitaifa wa uendeshaji wa Elimu ya Awali unaozingatia viwango. Lengo la Mwongozo huo ni kufafanua viwango vya Elimu ya Awali kwani kwa sasa kuna mifumo mingi ambayo inahitaji uratibu wa karibu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi hao kusoma katika mazingira tulivu na salama yenye kusaidia kuinua ubora wa elimu na mafunzo;

(ii) itagharamia chakula kwa wanachuo 20,236 na Mafunzo kwa Vitendo (*Block Teaching Practice - BTP*) kwa wanachuo 12,782 katika Vyuo vya Serikali 35 vya Ualimu;

(iii) itafanya ufuatiliaji wa utoaji wa Elimu ya Awali na Msingi kwa kuzingatia matokeo ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Pili na la Nne pamoja na Mtihani wa kuhitimu Darasa la Saba;

(iv) itafanya ufuatiliaji wa uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza katika shule tatu za Msingi kwa kila kanda 11; na

(v) itafanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera zinazohusu Elimu ya Sekondari ili kuinua ubora wa Elimu itolewayo.

**Usimamizi wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

**78. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara itafanya yafuatayo:

(i) kutekeleza mpango wa Mtaala wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo wa Elimu (*Intergrated Program for Out of School Adolescent*-IPOSA)

wenye Stadi za Kisomo (KKK), Ufundi Stadi wa Awali (*Pre-Vocational*), Stadi za Maisha (*Life Skills*) na Ujasiriamali (*Enterprenuership*) kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

**Usimamizi wa Masuala Mtambuka katika Elimu**

**79.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kusimamia Masuala Mtambuka kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kuwajengea uwezo walimu wa malezi Shuleni na katika Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha stadi za utoaji wa Huduma ya Ushauri na Unasihi kwa wanafunzi, kwa lengo la kukabiliana na changamoto wanazopata;

(ii) kusambaza mwongozo wa utoaji Huduma ya Ushauri na Unasihi shuleni na katika Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha huduma hiyo; na

(iii) kuendesha mafunzo ya Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika mikoa kumi ya Tanzania Bara.

**Usimamizi wa Elimu Maalum**

**80. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kuwa Elimu ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania, Wizara kwa mwaka 2018/19 itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2018-2021 ili kuwawezesha wadau wa elimu kushiriki kwa ufanisi katika utekelezaji wake;

(ii) itafanya ufuatiliaji wa utoaji wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ili kuhakikisha kuwa wanafaidika na fursa za Elimu nchini; na

(iii) itaandaa mkakati maalumu wa kutoa Elimu maalumu utakaowezesha kupunguza changamoto za ufundishaji, ujifunzaji na utahini ambazo zinawakabili walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**81. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/2019 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

(i) kuratibu ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera kitakachojengwa

kwa ruzuku kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;

(ii) kuendelea na ujenzi wa chuo cha Mkoa cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Njombe na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Mikoa ya Rukwa, Simiyu na Geita; na

(iii) kugharamia chakula na mafunzo kwa vitendo (*Industrial Practical Training*) kwa wanafunzi 903 wa Chuo cha Ufundi Arusha.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**82. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Wizara imepanga kufanya yafuatayo:

(i) kuratibu Skolashipu za Wanafunzi wa Vyuo Vikuu zinazotolewa na nchi rafiki za Jumuiya ya Madola (Uingereza na New Zealand) pamoja na nchi nyingine zikiwemo China, Hungary, Russia, Algeria na Misri;

(ii) kufadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) kufuatilia maendeleo ya udahili na uandikishwaji wa Wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu na maendeleo ya utoaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo

ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(iv) kufuatilia utendaji wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (*African Centre of Excellence – [ACE II]*) ambavyo viko katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela; na

(v) kuendeleza ufadhili wa masomo ya wanataaluma kutoka katika Vyuo Vikuu vya Umma katika Shahada za Uzamili na Uzamivu katika nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

**Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kutambua, kujenga, kukuza na kuendeleza ubunifu kwa Watanzania katika nyanja ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kati. Katika mwaka 2018/19 Wizara itafanya yafuatayo:

(i) itatambua na kutegemeza teknolojia zinazozalishwa nchini na kuweka mazingira bora ya upatikanaji, uhaulishaji na uhawilishaji wa teknolojia hizo;

(ii) itaandaa mpango kazi wa kusimamia uanzishwaji na uimarishaji wa vituo vya kuendeleza teknolojia na ubunifu nchini;

(iii) itaandaa programu za kujenga uelewa kwa wananchi katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kujenga uchumi wa viwanda;

(iv) itasimamia na kuendeleza mchango wa teknolojia ya nyuklia katika maendeleo ya Taifa; na

(v) itaandaa mkakati wa kukuza ujuzi na utaalamu asilia wa wabunifu nchini katika ngazi zote ili kuibua vipaji vyao.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu**

**84. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) kuanza Ujenzi wa Ofisi ya Wizara Dodoma kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya watumishi ya kufanyia kazi;

(ii) kuandaa Mpango wa Wizara wa Kurithishana Madaraka (*Succession Plan)* kwa lengo la kuandaa watumishi kwa ajili ya kushika madaraka;

(iii) kutoa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo

wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (*Open Performance Review and Apraissal System* – OPRAS) kwa watumishi wa ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi;

(iv) kuendeleza matumizi ya Mfumo wa mawasiliano wa kupokea, kutunza na kusambaza nyaraka za ofisi (*E-Office*) kwa kuwapa mafunzo watumishi wa masjala ili kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yao; na

(v) kuhakiki vyeti vya elimu na taaluma kwa waombaji wa kazi ya ualimu katika shule za Serikali kulingana na vibali vitakavyotolewa kwa lengo la kuhakikisha kuwa watakaoajiriwa wanakidhi vigezo vya Muundo wa Utumishi wa Kada za Walimu.

**Usimamizi wa Rasilimali za Wizara**

**85. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kitatekeleza yafuatayo:

(i) kukagua Mapato na Matumizi ya Wizara na taasisi zifuatazo; Vyuo vya Ualimu 15, Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za

Kanda 11, Vituo vya Elimu vya Uchapaji 2 (*PRESS A* na Kisomo Mwanza);

(ii) kukagua menejimenti ya rasilimaliwatu na malipo ya mishahara kwa watumishi wa Wizara;

(iii) kukagua taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba yote ya Wizara;

(iv) kukagua miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara;

(v) kukagua fedha zinazopelekwa katika Taasisi 6 za Wizara (HESLB, NECTA, NACTE, TEA, ADEM na TIE);

(vi) kukagua mifumo ya utawala bora na uendeshaji wa Wizara; na

(vii) kukagua utunzaji wa mali za Wizara *(Asset Management)*.

**URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Taasisi na Wakala tunazozisimamia. Shughuli zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

**87. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19 Taasisi itatekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kuboresha mtaala wa Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne na mtaala wa Elimu ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada;

(ii) kuendelea na uandishi wa vitabu vya kiada kwa Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita na Moduli/Vibutu vya Elimu ya Ualimu pamoja na kuandaa maudhui ya kielekroniki kwa Darasa la Kwanza na la Pili;

(iii) kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa Elimumsingi kwa kutumia mtaala ulioboreshwa;

(iv) kurusha hewani vipindi vya Vikaragosi (*Cartoons)* kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na la Pili, kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu( KKK);

(v) kuandika vitabu vya hadithi vya shule za msingi; kufanya uhakiki na tathmini ya vitabu vya ziada na maudhui ya kielektroniki; na

(vi) kuandika na kuchapa Mitaala, Mihtasari na Moduli za Mafunzo kwa ngazi ya Cheti na Stashahada ya Ualimu.

**Baraza la Mitihani la Tanzania**

**88. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Baraza litatekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,609,247 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2018;

(ii) kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 965,255 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Septemba, 2018;

(iii) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 547,846 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2018;

(iv) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 440,382 pamoja na mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,500 wanaotarajiwa kufanya Mitihani hiyo mwezi Novemba, 2018;

(v) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 80,628 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2019;

(vi) kuendesha Mtihani wa Cheti na Stashahada ya Ualimu kwa watahiniwa 12,500 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2019;

(vii) kuendesha upimaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 10,250 wa Darasa la Pili;

(viii) kutoa na kusambaza vyeti kwa wahitimu wa Darasa la Saba;

(ix) kuandaa Miundo ya Mitihani (*Examination Format)* ya Kidato cha Pili, Kidato cha Nne, na Kidato cha Sita kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa elimu; na

(x) kuchapa na kusambaza vitabu vya tathmini ya Upimaji na mitihani ya kitaifa katika ngazi zote za Elimu ya Msingi na Sekondari.

**Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2018/19 Mamlaka imetenga kiasi cha **Shilingi 9,750,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) kuwezesha ujenzi wa nyumba 15 za walimu katika shule za sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi;

(ii) kuwezesha ujenzi wa madarasa 300 kwenye shule za msingi 60 zenye uhitaji mkubwa;

(iii) kuwezesha ujenzi wa mabweni 10 ya wasichana kwenye Shule za Sekondari zilizo kwenye maeneo magumu kufikika; na

(iv) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi.

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**90.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Taasisi imetenga jumla ya **Shilingi 2,852,474,000** kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo;

(i) kuandaa na kutoa mafunzo ya wawezeshaji wa programu za kisomo na kufanya kampeni ya kisomo kwa kanda za kitaaluma kujenga na kuweka mtandao wa TEHAMA ili kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji wa programu za elimu na mafunzo za TEWW;

(ii) kuongeza wanafunzi wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka 10,420 mpaka 12,000 kwa kufungua vituo kwenye mikoa mipya mitano ya Songwe, Geita, Katavi, Njombe na Simiyu;

(iii) kuimarisha uwezo wa Maktaba ya TEWW kwa kuweka mifumo ya TEHAMA itakayotumika katika ufundishaji na ujifunzaji na kuongeza eneo la kujisomea;

(iv) kufanya utafiti katika programu ya elimu nje ya mfumo rasmi ili kubainisha hali ya sasa ya vijana na watu wazima wasio na stadi za kisomo na kupata taarifa mahususi za kupanga mikakati ya kuwapatia elimu stahiki; na

(v) kukarabati na kufanya upanuzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Kampasi ya Morogoro.

**Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**91. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Mamlaka imetenga **Shilingi 39,491,923,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu katika vyuo vya Ufundi Stadi nchini kutoka 200,000 mpaka 250,000;

(ii) kuanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Kagera**;**

(iii) kujenga karakana 3 katika vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Manyara;

(iv) kuendelea na ujenzi wa karakana 2 za ufundi wa zana za kilimo na ufundi wa uungaji vyuma katika chuo cha Ufundi Stadi Arusha;

(v) kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya za Chunya, Kilindi, Nyasa na Ukerewe;

(vi) kumalizia ujenzi wa madarasa 2 na mabweni 2 katika chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Makete;

(vii) kuweka vifaa vya mafunzo katika karakana ya Kisasa ya Useremala katika Chuo cha VETA Dodoma;

(viii) kuwajengea uwezo walimu wa ufundi stadi ili kuboresha ujuzi wao uendane na mabadiliko ya kiteknolojia;

(ix) kuimarisha ubora wa ukaguzi "quality audit" katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi vilivyosajiliwa na VETA katika Kanda mbili;

(x) kutoa ithibati na usajili wa kudumu kwa Vyuo vya Ufundi Stadi vitakavyokidhi vigezo vilivyowekwa;

(xi) kutoa mafunzo ya Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro kwa walimu 700 katika ngazi ya cheti na stashahada; na

(xii) kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETMIS) ili kudhibiti taarifa za mafunzo na watumishi.

**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

**92.** **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2018/19 Baraza litaendelea kuboresha Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kukagua na kusajili Vyuo vya Ufundi vitakavyokidhi sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, pamoja na kukagua na kutoa miongozo itakayoviwezesha vyuo kupata ithibati kamili endapo vitakidhi vigezo vilivyowekwa;

(ii) kufuatilia na kutathimini vyuo 400 vya Elimu ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yana ubora na yanakidhi soko la ajira; na

(iii) kuratibu uandaaji wa Mitaala 45, kuhuisha Mitaala 6 na Kukuza Mitaala 10 ya Kitaifa inayozingatia umahiri katika vyuo vya Elimu na Ufundi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu**

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Wakala unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kudahili walimu 2,300 watakaosoma Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) na Stashahada ya Ukaguzi wa Shule;

(ii) kudahili Walimu Wakuu 486 kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Songwe na Njombe watakaosoma Astashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Shule za Msingi ili kuwajengea uwezo wa kusimamia Shule zao; na

(iii) kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa wajumbe 2,115 wa Bodi za Shule za Sekondari kuhusu Nyaraka na Miongozo mbalimbali ya Elimu; Uongozi na Utawala wa Shule; Muundo na Majukumu ya Bodi za Shule; Usimamizi wa Fedha na Manunuzi; pamoja na Uaandaaji wa Mpango wa Maendeleo ya Shule.

**Bodi ya Huduma za Maktaba**

**94. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Bodi itatekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;

(ii) kutoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka katika ngazi ya Cheti cha Msingi (NTA 4) wanafunzi 350, Cheti (NTA 5) wanafunzi 320 na Stashahada (NTA 6) wanafunzi 340; na

(iii) upanuzi wa Maktaba ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka cha Bagamoyo na jengo la Maktaba ya Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa Wananchi wa Mikoa hiyo kupata huduma za Maktaba. Kiasi cha **Shilingi 2,500,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**95. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Bodi imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) kuunganisha na kuifanya mifumo ya upangaji, ulipaji na urejeshaji mikopo kujiendesha (*Full automation and integration of systems);*

(ii) kutoa mikopo ya **Shilingi billioni 427** kwa wanafunzi wapatao **123,285**, kati yao wakiwemo wanafunzi wa mwaka wa kwanza **40,544** na wanafunzi wanaoendelea na masomo wapatao **82,741;**

(iii) kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa ukusanyaji wa mikopo iliyoiva na kukusanya **Sh. 157,700,000,000.00** kwa mwaka;

(iv) kuendelea kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kurejesha mikopo kutoka kwa wanufaika, pamoja na kuujulisha umma kuhusiana na mwongozo wa utoaji mikopo kwa kuzingatia mahitaji ya kitaifa, sifa za waombaji na tarehe ya kuanza kupokea maombi ya mikopo; na

(v) kutoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye vigezo vya kupata mikopo na ruzuku hizo.

**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**96. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Tume itafanya yafuatayo:

(i) kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa Kupitia Mifumo na Miongozo mbalimbali inayotumika kusimamia Uthibiti na Ithibati ya Elimu ya Juu nchini;

(ii) kukagua Vyuo 20 vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuhakiki ubora wake;

(iii) kufanya tathmini kwa programu 100 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini na kuzisajili zitakazokidhi vigezo;

(iv) kufanya tathmini na kutambua Tuzo 2,500 za ngazi za Shahada zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyopo

nchi za nje;

(v) kuboresha Mfumo wa kutumia TEHAMA katika utoaji na ukusanyaji taarifa kutoka vyuo vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji;

(vi) kushiriki katika kongamano na mikutano ihusuyo uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini;

(vii) kuratibu Maonyesho ya 13 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu vyuo na programu mbalimbali zitolewazo; na

(viii) kuhakiki wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliodahiliwa katika vyuo vya Elimu ya Juu ili kujiridhisha kama wamekidhi vigezo vya kudahiliwa katika programu husika.

**Vyuo vya Elimu ya Juu**

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**97. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kitatekeleza yafuatayo:

(i) kudahili jumla ya wanafunzi 17,220 wa fani mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao; wanafunzi 4,000 watadahiliwa katika fani ya Cheti, wanafunzi 3,000 Stashahada, wanafunzi 8,000 Shahada ya Kwanza, wanafunzi 2,100 Shahada ya Uzamili na 120 Shahada ya Uzamivu; na

(ii) kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika nyanja za mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano.

**Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

98. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kitatekeleza yafuatayo:

(i) kusajili wanafunzi 4,386 wakiwemo wanafunzi 716 wa Astashahada, 1,074 wa Stashahada, 2,390 wa Shahada, 40 wa Stashahada ya Uzamili, 133 wa Shahada ya Umahiri na 33 Shahada ya Uzamivu;

(ii) kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua watumiaji 2,500 kwa wakati mmoja, ujenzi huu umetengewa **Shilingi 2,000,000,000**; na

(iii) kuanzisha Stashahada 2, Shahada za Kwanza 2 na Shahada za Uzamili 2 kwa lengo la kupanua wigo wa programu za mafunzo ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kukidhi mahitaji ya sasa.

**Chuo Kikuu cha Ardhi**

99. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo Kikuu cha Ardhi kitatekeleza yafuatayo:

(i) kufanya miradi ya tafiti 30 hususan katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo. Aidha, Chuo kitatoa huduma za ushauri kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi,

upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi kwa Wilaya 5 na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa maafisa watendaji wa halmashauri pamoja na wananchi;

(ii) kuendelea kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ardhi (*Lands Building*) na kuliunganisha na mfumo wa maji; na ujenzi wa Maabara (*Multi-Purpose Laboratory*) na kukarabati karakana, nyumba za watumishi na madarasa. **Shilingi Billioni 2.5** zimetengwa kwa ajili ya shughuli hii;

(iii) kudahili wanafunzi 4,700;

(iv) kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 53; wanataaluma wakiwemo 28 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na 25 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili;

(v) kumalizia kupitia na kuboresha mitaala 84 ya Chuo na kuiwasilisha Tume ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya kuidhinishwa;

(vi) kufanya miradi ya utafiti 30 katika maeneo ya usimamizi wa Ardhi na mazingira, makazi na majengo;

(vii) kuandaa machapisho 154 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi, na majengo; na

(viii) kutoa huduma za jamii juu ya matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi kwa Wilaya tano (5) kwa maafisa watendaji wa Halmashauri pamoja na wananchi;

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**100.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuongeza idadi ya miradi ya utafiti yenye ufadhili wa washirika wa maendeleo kutoka 209 hadi 250 (ongezeko la asilimia 20);

(ii) kuandaa "Juma la Utafiti" na kuonyesha matokeo ya tafiti za Chuo kupitia majarida, magazeti, runinga na redio; kitatoa mafunzo maalum ya utafiti na uchapishaji kwa wanataaluma 80 na wanafunzi 80 wa shahada za uzamili; na kitapanua wigo wa kutangaza huduma za ushauri kwa njia mbalimbali zikiwemo kushiriki maonesho ya kitaifa na kimataifa na kutumia runinga, magazeti, machapisho na vipeperushi;

(iii) kuongeza idadi ya machapisho katika majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka 354 kwa sasa hadi 390 (ongezeko la asilimia 10);

(iv) kuongeza idadi ya majarida ya kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka 9 kwa sasa hadi 24 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao;

(v) kununua vitabu, samani na mashubaka kwa ajili ya Maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(vi) kuongeza vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(vii) kufanya upanuzi wa Hosteli za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo zimetengwa **Shilingi Billioni 2**.

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**101.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kudahili wanafunzi 12,269 wa Shahada ya Kwanza 10,487 wa Stashahada 1,581 na wa Astashahada 201; na

(ii) kitafanya tafiti kumi (10) katika Nyanja mbalimbali na kitatoa huduma za ushauri kwa watakaohitaji. Vilevile, Chuo kinategemea kuwa na

mahusiano (collaborations) na taasisi mbili (2) mpya za kimataifa.

**Chuo Kikuu cha Mzumbe**

**102.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kufanya tafiti katika maeneo 21. Aidha, kitatoa mafunzo na kutekeleza kazi za ushauri wa kitaalamu katika maeneo 37 ya Menejimenti, Uongozi na Sayansi ya Jamii;

(ii) kudahili wanafunzi wapya 4,712 (Cheti 173, Astashahada 418, Shahada ya kwanza 3,202, Shahada ya Umahiri 909 na Shahada ya Uzamivu 10);

(iii) kuendeleza ujenzi na uwekaji samani katika jengo la madarasa na utawala, Kampasi ya Mbeya ambapo jumla ya **Shilingi 2,500,000,000.00** zimetengwa kwa mwaka 2018/19;

(iv) kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya eneo la Iwambi, Kampasi ya Mbeya;

(v) kuboresha huduma na miundombinu ya TEHAMA;

(vi) kufadhili wanataluma 8 kusoma

masomo ya Shahada ya Umahiri na 10 kusoma masomo ya Shahada ya Uzamivu.

**Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**103.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo;

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa Kwanza wakiwemo wanafunzi wa Shahada za Kwanza kutoka 3,250 hadi 3,700 Shahada za juu (Uzamili na Uzamivu) kutoka 171 hadi kufika 400. Ongezeko hili ni kutokana na kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ambapo jumla ya **Shilingi 8,000,000,000.00** zimetengwa kwa mwaka 2018/19;

(ii) kuendesha programu 80 za utoaji wa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa washiriki 350 wakiwemo wakulima, maafisa ugani na watafiti;

(iii) kuongeza ushirikiano na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi;

(iv) kuvijengea uwezo wa kifedha na kitaalamu vitengo vya uzalishaji ili viweze kuongeza mapato ya ndani ya Chuo kwa asilimia kumi (10%); na

(v) kufanya tafiti mbalimbali zaidi ya 150 kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, Chuo kitatoa huduma ya elimu na ushauri kwa wakulima 2,500 kwa kutumia mbinu mbalimbali kama semina, kozi fupi, warsha, runinga na redio kwa lengo la kupunguza umasikini kwa wananchi. Chuo kitaendelea kujenga na kukarabati Miundombinu ya Chuo na kutekeleza miradi ya tafiti.

**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**104.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa shahada ya kwanza na ya uzamili kwa asilimia 50;

(ii) kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kujifunzia kutoka asilimia 10 hadi kufikia asilimia 20;

(iii) kutengeneza vigezo vya kupima uadilifu kwa wanafunzi (*Professionalism Assessment Tool*);

(iv) kufundisha walimu vinara *(Health Professional Educators)* kwa kila skuli;

(v) kutengeneza mpango wa kuboresha huduma kwa wagonjwa *(Patient Centered Service Strategy)* na kuboresha mfumo wa huduma na taarifa kwa wagonjwa *(Health Information Management System);*

(vi) kukamilisha uandaaji wa mpango wa uzalishaji mali wa hospitali ya kufundishia na taaluma – Mloganzila;

(vii) kuongeza uwiano wa wanafunzi wa kike kufikia asilimia 40;

(viii) kukamilisha ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo awamu ya I *(Cardiovacular Centre of Excellence)* katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila kwa tengeo la **Shilingi 1,800,000,000**;

(ix) kutoa mafunzo kwa makundi tafiti katika skuli *(Research Clusters);*

(x) kuanzisha tafiti mpya 2 na kutoa ushauri wa taaluma tiba 5 kwa kila skuli;

(xi) kufanya mkutano wa kitaaluma wa sita *($6^{th}$ MUHAS Scientific Conference)* ili kutoa taarifa za tafiti; *na*

(xii) kuendelea kufanya tafiti za magonjwa ambukizi *(HIV Vaccine Trial, Intergrated Biobehavioral Surveys For Key Population, Prep for HIV, Malaria Na Tuberculosis),* magonjwa yasiyoambukiza *(Non-Communicable Diseases),* magonjwa yasiyopewa kipaumbele na *(Neglected Tropical Diseases) na* mfumo wa afya (*Health System Research*).

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**105. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4,066 hadi 5,338 na kuboresha maktaba moja ya Chuo;

(ii) kutoa mafunzo ya kina katika programu za elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali, ngazi ya kati mpaka ngazi ya juu ya kada ya ualimu;

(iii) kurekebisha na kuboresha mitaala katika programu za elimu na kutekeleza utafiti na uzinduzi wa programu ya elimu ya mazoezi na sayansi ya michezo;

(iv) kukamilisha ujenzi wa maabara ya sayansi na kompyuta, kwa tengeo la shilingi billioni **2;**

(v) kusomesha watumishi 90 katika mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya Kwanza, Umahiri na Uzamivu;

(vi) kutekeleza miradi 13 ya utafiti *(Research Projects*) na utoaji ushauri (*Consultancy)* ambapo miradi 7 ni endelevu na miradi 6 itakuwa mipya; na

(vii) kuchapisha machapisho 50 kwenye majarida mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na kutoa chapisho la tatu la jarida la Chuo liitwalo *Mkwawa Journal of Education and Development (MJED).*

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

**106. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo;

(i) kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 2,100 kati ya hao 700 wanatarajiwa kuwa wa fani ya Sayansi;

(ii) kuandaa mitaala 4 mipya ya Shahada za Awali na Umahiri; na

(iii) ujenzi wa Jengo la Makazi ya Wanataaluma Watafiti pamoja na kujenga madarasa na kuweka mifumo ya kiusalama na miundombinu ya TEHAMA chuoni kazi hii imewekewa tengeo la **Shilingi billioni 2.**

**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**107.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuboresha elimu na utendaji kazi kwa watumishi kwa kuendesha mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 12 wa taaluma na wafanyakazi 6 wa utawala na mafunzo ya muda mfupi kwa wahadhiri 12 na wafanyakazi wa utawala 10;

(ii) kuanza ujenzi wa jengo la maktaba Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ambapo **Shilingi millioni 500** zimetengwa; na

(iii) kujenga Bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar ambapo kiasi cha **Shilingi millioni 500** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi.

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**108.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Chuo kitatekeleza yafuatayo;

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 4,209 kwa mwaka wa masomo 2017/2018 hadi kufikia wanafunzi 4,500 kwa mwaka wa masomo 2018/2019;

(ii) kuanza kutoa mafunzo ya uhandisi katika ngazi ya stashahada katika Kampasi ya Rukwa kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Mafunzo yataanza kutolewa katika fani ya Uhandisi Barabara;

(iii) kuendelea na kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 ili kukidhi mahitaji ya huduma bora za maktaba kwa wanafunzi na wahadhiri, ambapo **Shilingi billioni 2** zimetengwa kutekeleza kazi hii;

(iv) kuendelea kuongeza matumizi ya

nishati mbadala ili kuwa na vyanzo endelevu vya nishati kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chuo;

(v) kufanya tathmini ya mali za wananchi katika eneo ambalo limeainishwa kuongezwa katika Kampasi ya Rukwa ili lifikie ukubwa wa hekta 500. Kiasi cha **Shilingi 20,000,000** kutoka mapato ya ndani kimetengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli hiyo;

(vi) kuanzisha bustani ya mimea kwa matumizi ya kitaaluma na kuleta ustawi wa mazingira ya Chuo. Kiasi cha **Shilingi 114,079,093** kutoka mapato ya ndani ambapo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 50,000,000** ni msaada kutoka *Tanzania Forest Fund;*

(vii) kujenga jengo lenye vyumba viwili vya madarasa vitakavyokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 kwa pamoja kwa kutumia fedha zinazotokana na mapato ya Chuo ya ndani ambapo kiasi cha **Shilingi 270,000,000** zimetengwa;

(viii) kugharamia chakula kwa wanafunzi 338 na mafunzo kwa vitendo *(Industrial Practical Training)* kwa wanafunzi 268 wa Taasisi ya Sayansi

na Teknolojia Mbeya;

(ix) kufanya tafiti zinazolenga kuongeza ubunifu na kuendelea kutoa ushauri elekezi katika nyanja za sayansi na teknolojia ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo katika jamii;

(x) kuunda gari dogo kwa ajili ya kubebea mizigo midogo midogo kwa lengo la kurahisisha kazi za uvunaji kwa wakulima wa viazi. Mfano wa Gari umeundwa na unaendelea kuboreshwa ili kukidhi maoni ya wadau mbalimbali. Faida ya gari hilo litasaidia huduma za usafirishaji wa mizigo ambayo haiendi umbali mrefu. Kiasi cha **Shilingi 5,527,000** kutoka mapato ya ndani kimetengwa kwa kazi hiyo;

(xi) kuandaa mfumo wa kuzalisha gesi kwa kutumia samadi kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuwasha taa katika maeneo ya vijijini. Mfumo wa uzalishaji wa gesi kwa ajili ya kupikia kutokana na samadi uliundwa na kujaribiwa katika maeneo ya Mbozi. Mfumo huu unasaidia kupunguza uharibifu wa misitu na kupunguza

gharama za maisha kwa wananchi wenye mifugo ambao wanaweza kupata njia mbadala ya nishati kwa kutumia samadi; na

(xii) kuunda mashine kwa ajili ya kupukuchua mazao mbalimbali. Mashine hii itasaidia kupunguza upotevu wa chakula wakati wa kupukuchua na pia kupunguza muda wa kupukuchua mazao na hivyo kumpa mkulima muda mwingi katika shughuli nyingine za kiuchumi. Kiasi cha **Shilingi 3,000,000** kimetengwa.

**Chuo cha Ufundi Arusha**

**109.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kufanya utafiti wa matumizi bora ya maji katika kilimo cha mpunga kwa kushirikiana na *Japan International Research Centre for Agricultural Sciences* (*JIRCAS*);

(ii) kufanya utafiti wa mradi wa umeme Wilayani Mbulu chini ya ufadhili wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ambapo umeme utakaozalishwa utahudumia vijiji viwili vya Kwermusl na Amoa;

(iii) kufanya utafiti wa majaribio ya mitambo midogo iliyoundwa ya kuzalisha umeme utokanao na nishati ya Maji katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa;

(iv) kuendelea na utafiti kuhusu uundaji wa helikopta;

(v) kuanza ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme utokanao na nishati ya maji katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa kwa kushirikiana na mwekezaji mwenza;

(vi) kukamilisha ukarabati na ufungaji vifaa katika karakana 5 za Chuo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo karakana zitakazopata vifaa ni pamoja na karakana 2 za uhandisi mitambo, karakana moja ya useremala na karakana 2 za uhandisi magari kwa tengeo la **Shilingi 100,000,000** fedha za ndani;

(vii) kujenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 250 kwa pamoja kwa tengeo la **Shilingi 250,000,000** fedha za ndani;

(viii) kujenga na kukarabati miundombinu ya madarasa, maabara na karakana katika vituo vya mafunzo vya Kikuletwa na Oljoro kwa tengeo la **Shilingi 1,945,319,000.00**;

(ix) kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa wanafunzi wapatao 500 kwa utaratibu wa Skimu za Vocha za Mafunzo kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na

(x) kukamilisha ufungaji wa mtandao wa intaneti (*Local Area Network*) katika majengo yote ya Chuo kutoka kwenye Mkongo wa Taifa ili kuboresha utoaji wa mafunzo kupitia TEHAMA ambapo kiasi cha **Shilingi 600,000,000** hela za ndani zimetengwa.

**110.** **Mheshimiwa Spika,** vile vile Chuo cha Ufundi Arusha kitatoa ushauri wa kitaalamu kuhusu:

(i) tathmini ya uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara, ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi; na

(ii) ufungaji wa *Solar PV* kupitia mradi wa *Sustainable Solar Market Packages* (*SSMP*).

**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**111. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili wanafunzi wapya 1,700 na kuendelea kuhudumia wanafunzi 2,900; wanaoendelea hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 4,600;

(ii) kukamilisha upanuzi wa jengo la Maktaba kwa kutumia mapato ya ndani ambapo **Shilingi 400,000,000.00** zimetengwa;

(iii) kuweka samani za ndani na miundombinu na vifaa vya TEHAMA katika jengo jipya ambapo zimetengwa **Shilingi 1,000,000,000** fedha za ndani;

(iv) kuanzisha kozi mpya za Shahada ya Uhandisi katika Madini na Shahada ya Umahiri katika Uhandisi wa Nishati Endelevu;

(v) kuendelea kuhudumia wafanyakazi 36 walioko masomoni;

(vi) kupeleka wanafunzi 550 mafunzo ya vitendo viwandani;

(vii) kuanzisha kozi ya Stashahada ya utengenezaji viatu na kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya kitaalam katika teknolojia ya ngozi katika Kampasi ya Mwanza; na

(viii) kuendelea na utoaji wa mafunzo ya ufundi mchundo na kuanza maandalizi ya kutoa mafunzo ya muda mrefu katika Kampasi ya Myunga.

**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha**

**112.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Taasisi itatekeleza yafuatayo:

(i) kudahili wanafunzi 215; Shahada ya uzamili 175 na Uzamivu 40;

(ii) kuhamasisha upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya kitafiti kwa kuandika maandiko yapatayo 48;

(iii) kuongeza idadi na mahusiano mazuri na wadau wetu wa kimataifa kutoka 24 hadi 30, wadau wa kanda ya afrika mashariki kutoka 29 hadi 35 na wadau wa ndani ya nchi kutoka 17 hadi 25;

(iv) kuanza ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja ambapo **Shilingi 1,000,000,000** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/19; na

(v) kukamilisha tafiti 12 zinazoendelea.

**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia**

**113.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kupima ardhi na kufuatilia upatikanaji wa Hati Miliki za ardhi ya Chuo kwa Kampasi za Butiama, Rorya na Serengeti;

(ii) kuanzisha programu 5 na kununua vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(iii) kuandaa mitaala 10 kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza, kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa na TCU;

(iv) kuimarisha shughuli za mafunzo na huduma za ugani kwa jamii za wakulima, wafugaji, wavuvi, na wachimbaji madini wadogowadogo walioko jirani na Chuo; na

(v) kuandaa michoro na mpango wa matumizi ya Ardhi kwa ajili ya Chuo kwa tengeo la **Shilingi 1,000,000,000**.

**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**114.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Tume imetenga jumla ya **Shilingi 9,680,000,000** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kuanzisha na kuendeleza Atamizi za Ubunifu katika Halmashauri za Mji wa Mbeya na Dodoma zinazolenga kukuza ubunifu kwa jumla ya vijana 50;

(ii) kuwatambua wagunduzi na wabunifu nchini na kuwawezesha kuendeleza ubunifu na ugunduzi wao kupitia mfuko wa MTUSATE. Tume itafadhili miradi 20 kwa kutumia Mwongozo ulioandaliwa ambao unaweza kupatikana Tume ya Sayansi na Teknolojia;

(iii) kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya kama *Bioteknolojia, Nanoteknolojia, Mekatroniksi* na *Bigdata* ili kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kuandaa na kufanya majukwaa ya majadiliano pamoja na kuhamasisha

jamii kupitia vyombo vya habari;

(iv) kuandaa vipindi na makala 42 zinazohusiana na masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU) na kuzisambaza katika Radio na Televisheni ili kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika kuboresha shughuli za kiuchumi na kijamii; na

(v) kuanzisha na kuendeleza kumbi za Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuchochea uanzishwaji wa kampuni za kiteknolojia ili kukuza ubunifu na kuongeza ajira kwa vijana.

**Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania**

**115.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Tume itatekeleza yafuatayo:

(i) kuanza ujenzi wa maabara ya Tume awamu ya pili ambayo itaboresha utoaji huduma, kuongeza mapato na ufanisi katika utendaji wa kazi za Tume ambapo kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** imetengwa;

(ii) kupokea na kutathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004;

(iii) kuendelea na ukaguzi wa migodi 6 (*Geita Gold Mine* - Geita, Bulyanhulu Gold Mine - Kahama, *North Mara Gold Mine* - Tarime, Buzwagi Gold Mine - Kahama, *Williamson Gold Mine* - Shinyinga, *Stami Gold* Tulawaka - *Biharamulo*) inayofanya kazi ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo;

(iv) kuendelea kukagua vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 150 ili kubaini hali ya usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla;

(v) kuendelea na usajili wa vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 1,045;

(vi) Kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi kwa Wafanyakazi 1,600;

(vii) kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo vinne na kuyahifadhi katika jengo maalumu (*Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF*) lililopo Arusha;

(viii) kupima kiasi cha mionzi katika sampuli angalau 6,000 za vyakula na mbolea;

(ix) kuimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 24 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine;

(x) kuendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga *(Radionuclide Monitoring Station-TZP-RN64)* kilichopo katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty* (CTBT) *for Non Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons;*

(xi) kuendelea kuratibu miradi mipya sita (6) ya kitaifa na miradi 30 ya kikanda ambayo itagharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency-IAEA)*;

(xii) kufanya kaguzi kwenye vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyoayonishwa *(Non-Ionizing Radiation)* mfano minara ya simu, redio, runinga, na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika; na

(xiii) kufungua ofisi za Tume katika kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Mkoa wa Mbeya na Kanda ya ziwa Mkoa wa Mwanza. Vigezo vinavyotumika kuchagua kanda ni uwepo wa vyanzo vya mionzi.

## MALENGO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2018/19

### Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu)

**116. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R) kwa mwaka 2018/19 imetenga kiasi cha **Shilingi 140,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kutoa motisha kwa Halmashauri zote kutokana na utekelezaji wa vigezo vya EP4R, Ufuatiliaji na Tathmini ya Uendeshaji wa Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu;

(ii) kutoa Motisha kwa shule za Msingi na Sekondari zilizofanya vizuri na zilizoongeza kiwango cha ufaulu katika Mitihani ya Taifa ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne 2018;

(iii) kujenga madarasa 2,000 na matundu ya vyoo 2,000 kwa Shule za Msingi na Sekondari;

(iv) kujenga mabwalo kwa shule 85 zilizopanuliwa kwa ajili ya kudahili wanafunzi wa Kidato cha Tano;

(v) kununua vifaa vya Maabara awamu ya pili kwa shule 1,800 za Sekondari za Wananchi;

(vi) kukarabati Shule Kongwe 25 za Sekondari ambazo ni; Arusha, Weruweru, Shinyanga, Rungwe, Mawenzi, Bukoba, Mara, Mtwara Wasichana, Lyamungo, Masasi Wasichana, Lindi, Kilosa, Machame Wasichana, Sumbawanga, Tarime, Kibasila, Tunduru, Tumaini, Pamba, Mbeya Kutwa, Moshi Wavulana, Ifunda Wasichana, Iringa Wasichana, Ashira, na Mwanza Sekondari;

(vii) kukarabati na kupanua Vyuo 8 vya Ualimu ambavyo ni Bustani, Vikindu, Mtwara Kawaida, Mtwara Ufundi, Singachini, Monduli, Bunda na Katoke; na

(viii) kununua magari 20 kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu.

**Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK**

**117.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (*Literacy* and *Numeracy Education Support-LANES*) kwa tengeo la **Shilingi 4,000,000,000** kwa kufanya yafuatayo:

(i) kufanya tathmini ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikakati ya Sekta ya Elimu;

(ii) kufanya tathmini ya mwisho ya utekelezaji wa shughuli za Programu ya LANES pamoja na Sekta ya Elimu (*Joint Education Sector Review - JESR*);

(iii) kuwezesha kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji cha Wizara ili kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za programu ya LANES; na

(iv) kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**118.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itatekeleza yafuatayo: -

(i) kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Njombe na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Simiyu, Geita na Rukwa ambapo kiasi cha **Shilingi 24,500,000,000** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo;

(ii) kuanza ujenzi katika Vyuo vya Ualimu 6 vya Dakawa, Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Butimba ambapo **Shilingi 5,450,000,000** zimetengwa kwa ujenzi huo; na

(iii) kuanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera chini ya ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.99 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo.

**Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu**

**119.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu itaendelea na ujenzi na ukarabati

wa vyuo vinne vya Ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali kwa tengeo la **Shilingi 12,370,0451,500**.

**Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu**

**120.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu imetenga jumla ya **Shilingi 20,241,960,000** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) kununua vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia kwa vyuo 35 vya Ualimu na vifaa vya Elimu Maalum kwa Vyuo vya Patandi, Mtwara Ufundi na Mpwapwa;

(ii) kuimarisha Mifumo ya TEHAMA, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa Vyuo vya Ualimu na Kuviunganisha katika Mkongo wa Taifa;

(iii) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga na kukarabati maktaba za Vyuo 8 vya Ualimu ambavyo ni Bustani, Vikindu, Mtwara Kawaida, Mtwara Ufundi, Murutunguru, Monduli na Bunda;

(iv) kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 821;

(v) kutoa mafunzo Kazini kwa wakufunzi 323 wa masomo ya Lugha, 162 wa Elimu ya Awali, 279 wa Sayansi, 132 wa Hisabati, 381 wa Sayansi ya Jamii na 162 wa Elimu ya Afya;

(vi) kuandaa mfumo wa mawasiliano na utunzaji taarifa za Elimu ya Ualimu (Kanzidata);

(vii) kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Hisabati ya Korogwe *Maths Project* na kutoa mafunzo kwa Walimu 200 wa somo la Hisabati wa shule za Msingi na Sekondari;

(viii) kuandaa Mkakati wa Jinsia na kutoa Elimu ya Jinsia kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

(ix) kuwezesha uendeshaji wa shughuli za mradi na kufanya ufuatiliaji na tathmini;

(x) kutoa ufadhili kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu 500 wa fani za Sayansi, Kilimo na Ufundi kusomea *Postgraduate* Diploma ya Ualimu ili waweze kuwa Walimu wa Sayansi wa Shule za Sekondari; na

(xi) kutoa ufadhili kwa Wakufunzi wa Chuo cha Ualimu Patandi

kujiendeleza katika ngazi ya Shahada ya Pili kwenye Elimu Maalum.

**Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni:**

**121.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara imetenga jumla ya **Shilingi 17,033,235,000** kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

(i) kujenga miundombinu ya Maji na Vyoo katika Shule za msingi 500;

(ii) kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa pamoja wa miundombinu ya vyoo na maji kwa kuzingatia mwongozo wa SWASH kwa kushirikiana na Wizara zinazotekeleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira ili kubaini mafanikio, changamoto katika kutekeleza Kampeni hii na kutoa ushauri stahiki; na

(iii) kutoa Elimu kuhusu utumiaji wa mwongozo wa SWASH kwa Wathibiti Ubora wa Shule na Waratibu wa SWASH wa Halmashauri na Mikoa ili waweze kukusanya takwimu za SWASH na kutoa taarifa kwa kutumia mfumo kila robo ya mwaka.

**Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (*Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP):***

**122.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) kujenga shule mpya za Mikoa katika Mikoa 7 ambapo jumla ya **Shilingi 21,000,000,000** zimetengwa;

(ii) kujenga nyumba za walimu 8 kwa kila shule katika shule mpya 7 za Mikoa ya Geita, Njombe, Lindi, Singida, Katavi, Ruvuma na Manyara ambapo jumla ya **Shilingi 2,800,000,000.00** zimetengwa**;** na

(iii) kununua samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule mpya 7 ambapo jumla ya **Shilingi 700,000,000.00** zimetengwa.

**Mradi wa TANZIS (*Tanzania Innovation Systems*):**

**123.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara itaanza kutekeleza yafuatayo kwa tengeo la **Shilingi 6,589,351,000**:-

(i) kuibua na kutambua wabunifu 70 mahiri Tanzania, kutoka makundi saba (Vyuo Vikuu, Ufundi Stadi,

Ufundi wa Kati, Atamizi na Kumbi za Ubunifu, Taasisi za Utafiti, Viwanda na Shule za Sekondari) ambayo kila kundi moja litatoa wabunifu 10 kwa lengo la kusaidia kukuza ujuzi utakaowezesha kujenga Tanzania ya Viwanda;

(ii) kuimarisha mazingira ya ubunifu kwa kuwasaidia wabunifu wachanga kupata vifaa na msaada wa kitaalam ili kuyaendeleza mawazo yao katika mazingira halisi ya kibiashara na kuonekana katika jamii;

(iii) kuwaunganisha wabunifu wenye taaluma mbalimbali na kuwapa mtaji ili waweze kutatua changamoto mbalimbali hasa katika maeneo ya viwanda vilivyopo nchini ili vifanye kazi kwa ufanisi;

(iv) kuwapatia nafasi wabunifu wachanga, wataalamu vyuoni, wataalamu katika sekta ya umma na sekta binafsi, kutembelea nchi ya Finland ili kujifunza mawazo mapya yatakayowezesha kuendeleza ubunifu wao; na

(v) kuhamasisha umma kuhusu mradi pamoja na kuwajengea uwezo waendelezaji wa ubunifu ili kuwa na uelewa wa pamoja.

## TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

**124.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Tume itatekeleza yafuatayo:

(i) kushirikisha Wizara, Taasisi za Umma, Taasisi binafsi pamoja na wadau mbalimbali katika kuchangia kuboresha maswala ya Elimu, Sayansi, Habari na Utamaduni; na

(ii) kuendelea kushiriki katika kazi za UNESCO haswa katika kupanga na kutekeleza program mbalimbali za UNESCO.

## D. SHUKRANI

**125.** **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa William Tate Olenasha (Mb) Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao wa karibu katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara yetu.

Napenda pia kuwashukuru, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara, Wanataaluma, Wanafunzi na Wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninatambua na kuthamini sana mchango wenu mzuri katika kuhakikisha kuwa sekta ya elimu nchini inaendelea kuimarika.

**126.** **Mheshimiwa Spika,** Washirika mbalimbali wa Maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru na kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Canada, China, Cuba, India, Italy, Hungary, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Uturuki na Ubelgiji. Aidha natoa shukrani za dhati kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

**127.** **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuyashukuru baadhi ya mashirika yaliyochangia katika kufanikisha Programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia: Aga Khan Education Service, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Commonwealth Secretariat, DAAD, DfID, Global Partnership

for Education, Inter University Council of East Africa (IUCEA), Japan International Cooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organisation (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Human Development Innovation Fund (HDiF), Swedish International Development Agency (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), UNESCO, UNICEF, USAID na WaterAid.

## E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

**128.** **Mheshimiwa Spika,** Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,406,469,626,000.00** ili kutekeleza majukumu yake**.**

**129.** **Mheshimiwa Spika,** Katika maombi haya:

(i) **Shilingi 476,500,224,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 406,267,946,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 70,232,278,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) **Shilingi 383,838,645,092.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 331,948,039,001.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 51,890,606,091.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(iii) **Shilingi 929,969,402,000.00 zinaombwa kwa** ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 618,969,400,000.00 ni** fedha za ndani na **Shilingi 311,000,002,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**130.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba jumla ya **Shilingi 666,855,000.00** ikiwa yote ni matumizi ya kawaida (**Mishahara** ni **334,562,000.00** na Matumizi mengineyo ni **Shilingi 332,293,000.00**).

**131.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya bajeti ya mafungu yote mawili (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 1,407,136,481,000.00.**

**132.** **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako

wewe pamoja na kwa waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza.

**KUTOA HOJA**

**133.** **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

## VIELELEZO

**Kielelezo Na. 1: Udahili wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma kwa Mwaka wa Masomo 2017/18**

| Na | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ardhi University | 459 | 666 | **1125** |
| 2 | Arusha Technical College | 48 | 168 | **216** |
| 3 | Center for Foreign Relations Dar es Salaam | 94 | 130 | **224** |
| 4 | College of African Wildlife Management Mweka | 32 | 72 | **104** |
| 5 | College of Business Education Mwanza | 16 | 27 | **43** |
| 6 | College of Business Education Dar es Salaam | 150 | 199 | **349** |
| 7 | College of Business Education Dodoma | 51 | 77 | **128** |
| 8 | Dar es Salaam Institute of Technology | 113 | 528 | **641** |
| 9 | Dar Es Salaam Maritime Institute | 12 | 72 | **84** |
| 10 | Dar es Salaam University College of Education | 708 | 1209 | **1917** |

| Na | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Eastern Africa Statistical Training Centre | 19 | 28 | **47** |
| 12 | Institute of Accountancy Arusha | 374 | 435 | **809** |
| 13 | Institute of Adult Education | 90 | 35 | **125** |
| 14 | Institute of Finance Management | 1506 | 1987 | **3493** |
| 15 | Institute of Finance Management Mwanza | 55 | 70 | **125** |
| 16 | Institute of Public Administration - Zanzibar | 56 | 43 | **99** |
| 17 | Institute of Rural Development Planning | 292 | 381 | **673** |
| 18 | Institute of Rural Development Planning- Lake Zone Centre (MWANZA) | 23 | 38 | **61** |
| 19 | Institute of Social Work | 301 | 164 | **465** |
| 20 | Institute of Tax Administration | 63 | 91 | **154** |
| 21 | Karume Institute of Science and Technology | 4 | 0 | **4** |

| Na | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 22 | Mbeya University of Science and Technology | 144 | 652 | **796** |
| 23 | Mkwawa University College of Education | 950 | 1693 | **2643** |
| 24 | Moshi Cooperative University | 363 | 463 | **826** |
| 25 | Muhimbili University of Health and Allied Sciences | 214 | 504 | **718** |
| 26 | Mzumbe University | 1277 | 1644 | **2921** |
| 27 | Mzumbe University (MU), Mbeya College | 625 | 693 | **1318** |
| 28 | National Institute of Transport | 401 | 1145 | **1546** |
| 29 | Open University of Tanzania | 524 | 1313 | **1837** |
| 30 | Sokoine University of Agriculture | 1229 | 2475 | **3704** |
| 31 | State University of Zanzibar | 216 | 234 | **450** |
| 32 | Tanzania Institute of Accountancy - MWANZA | 36 | 51 | **87** |
| 33 | Tanzania Institute of Accountancy - SINGIDA | 83 | 98 | **181** |

| Na | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 34 | Tanzania Institute of Accountancy (TIA) Mbeya | 157 | 178 | **335** |
| 35 | Tanzania Institute of Accountancy DSM | 563 | 583 | **1146** |
| 36 | Tanzania Public Service College Dar es Salaam Campus | 225 | 94 | **319** |
| 37 | Tengeru Institute of Community Development | 101 | 68 | **169** |
| 38 | The Mwalimu Nyerere Memorial Academy DSM | 890 | 1030 | **1920** |
| 39 | The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Zanzibar | 56 | 57 | **113** |
| 40 | University of Dar es Salaam | 3674 | 5394 | **9068** |
| 41 | University of Dodoma | 3257 | 5894 | **9151** |
| 42 | Water Institute | 40 | 118 | **158** |
| | **Jumla** | **19,491** | **30,801** | **50,292** |

**Kielelezo Na. 2: Udahili wa Vyuo vya Elimu ya Juu Visivyo vya Serikali kwa Mwaka wa Masomo 2017/18**

| Na | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | AbdulRahman Al-Sumait Memorial University | 75 | 72 | **147** |
| 2 | Aga Khan University | 31 | 6 | **37** |
| 3 | Catholic University of Health and Allied Sciences | 116 | 183 | **299** |
| 4 | Jordan University College | 108 | 155 | **263** |
| 5 | Josiah Kibira University College | 6 | 30 | **36** |
| 6 | Mount Meru University | 16 | 9 | **25** |
| 7 | MS Training Centre for Development Cooperation | 5 | 8 | **13** |
| 8 | Muslim University of Morogoro | 271 | 478 | **749** |
| 9 | Hubert Kairuki Memorial University | 138 | 146 | **284** |
| 10 | Mwenge Catholic University | 685 | 1339 | **2024** |
| 11 | Ruaha Catholic University | 417 | 562 | **979** |
| 12 | St. Augustine University in Tanzania Mbeya Center | 242 | 452 | **694** |

| Na | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 13 | St. Augustine University of Tanzania | 1523 | 2149 | **3672** |
| 14 | St. Augustine University of Tanzania(Arusha Centre) | 43 | 67 | **110** |
| 15 | St. Johns University of Tanzania | 461 | 714 | **1175** |
| 16 | St. Joseph University College of Health and Allied Sciences | 35 | 106 | **141** |
| 17 | Stefano Moshi Memorial University College | 70 | 93 | **163** |
| 18 | Stella Maris Mtwara University College | 92 | 206 | **298** |
| 19 | Teofilo Kisanji University Dar es Salaam College | 11 | 17 | **28** |
| 20 | Tumaini University Makumira | 347 | 408 | **755** |
| 21 | Tumaini University Dar es Salaam College | 368 | 324 | **692** |
| 22 | Unique Academy Dar es Salaam | 13 | 75 | **88** |
| 23 | University of Arusha | 111 | 90 | **201** |
| 24 | University of Iringa | 234 | 263 | **497** |
| 25 | Zanzibar University | 49 | 26 | **75** |
| | **Jumla** | **5,467** | **7,978** | **13,445** |

**Kielelezo 3: Ujenzi wa Nyumba 40 za Walimu kwenye sehemu zenye uhaba wa mkubwa wa Nyumba za Walimu na zisizofikika kwa urahisi**

Ujenzi wa nyumba 40 za walimu katika sehemu zenye uhaba mkubwa na zisizofikika kwa urahisi. Ujenzi unafanywa na Watumishi Housing Corporation (WHC).

| NA | MRADI | HALMASHAURI/ MKOA | HATUA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | Shule ya Sekondari Mvuti | Ilala MC-DAR ES SALAAM | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 2 | Shule ya Sekondari Mjawa | Kibiti DC- PWANI | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 3 | Shule ya Sekondari Msata | Chalinze DC- PWANI | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 4 | Shule ya Sekondari Iyogwe | Gairo DC- MOROGORO | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 5 | Shule ya Sekondari Mikangaula | Nanyumbu DC- MTWARA | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 6 | Shule ya Sekondari Likokona | Nanyumbu DC - MTWARA | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 7 | Shule ya Sekondari Duga | Mkinga DC -TANGA | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |

| NA | MRADI | HALMASHAURI/ MKOA | HATUA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 8 | Shule ya Sekondari Ndoleleji | Itilima DC - SIMIYU | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 9 | Shule ya Sekondari Isanzu | Mkalama DC -SINGIDA | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 10 | Shule ya Sekondari Ulel-ing'ombe | Kilosa DC- MOROGORO | Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa. |
| 11 | Shule ya Sekondari Kinamapula | Ushetu DC- SHINYANGA | Ujenzi umekamilika. |
| 12 | Shule ya Sekondari Luegu | Namtumbo DC- RUVUMA | Ujenzi umekamilika. |
| 13 | Shule ya Sekondari Kandawale | Kilwa DC- LINDI | Ujenzi umekamilika. |
| 14 | Shule ya Sekondari Kiangara | Liwale DC- LINDI | Ujenzi umekamilika. |
| 15 | Shule ya Sekondari Tandahimba | Mihambwe DC- MTWARA | Ujenzi umekamilika |
| 16 | Shule ya Sekondari Kasanga | Kalambo DC- RUKWA | Ujenzi upo katika hatua za awali kwa Force Account |

| NA | MRADI | HALMASHAURI/ MKOA | HATUA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 17 | Shule ya Sekondari Itebula | Uvinza DC-KIGOMA | Ujenzi upo katika hatua za ujenzi wa boma |
| 18 | Shule ya Sekondari Inyonga | Mlele DC-KATAVI | Ujenzi upo katika hatua za awali kwa Force Account |
| 19 | Shule ya Sekondari Manda | Ludewa DC-NJOMBE | Ujenzi upo hatua ya kumalizia |
| 20 | Shule ya Sekondari Uhambi-ngeto | Kilolo DC-IRINGA | Ujenzi upo hatua ya kumalizia kwa Force Account |
| 21 | Shule ya Sekondari Kapalala | Chunya DC-MBEYA | Ujenzi uko hatua za awali baada ya kuanza kwa Force Account |
| 22 | Shule ya Sekondari Sakami | Kondoa DC-DODOMA | Ujenzi umekamilika |
| 23 | Shule ya Sekondari Usunga | Sikonge DC-TABORA | Ujenzi upo katika hatua za awali baada ya kuanza kujengwa kwa Force Account |

| NA | MRADI | HALMASHAURI/ MKOA | HATUA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 24 | Shule ya Sekondari Nduruma | Ukerewe DC-MWANZA | Ujenzi upo katika hatua za mwisho. |
| 25 | Shule ya Sekondari Shishani | Magu DC-MWANZA | Ujenzi upo katika hatua ya kumalizia |
| 26 | Shule ya Sekondari Nyasato | Mbongwe DC-GEITA | Ujenzi upo katika hatua za awali. |
| 27 | Shule ya Sekondari Nyaluhande | Busega DC-SIMIYU | Ujenzi upo katika hatua za awali. |
| 28 | Shule ya Sekondari Mwasamba | Busega DC-SIMIYU | Ujenzi upo katika hatua ya kumalizia |
| 29 | Shule ya Sekondari Kisaka | Serengeti-MARA | Ujenzi upo katika hatua ya boma |
| 30 | Shule ya Sekondari Nyambureti | Serengeti DC-MARA | Ujenzi upo katika hatua ya boma |
| 31 | Shule ya Sekondari Kakunyu | Misenyi DC-KAGERA | Ujenzi upo katika hatua ya kupaua |
| 32 | Shule ya Sekondari Nemba | Biharamulo DC-KAGERA | Ujenzi upo katika hatua ya kupaua |

| NA | MRADI | HALMASHAURI/ MKOA | HATUA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 33 | Shule ya Sekondari Oldonyolen-gai | Monduli DC-ARUSHA | Ujenzi upo katika hatua ya kumalizia |
| 34 | Shule ya Sekondari Sale | Ngorongoro DC-ARUSHA | Ujenzi upo hatua za awali baada ya kupadilishwa kwenda Arash Sekondari |
| 35 | Shule ya Sekondari Eng'eno | Simanjiro DC-MANYARA | Ujenzi upo katika hatua za awali. |
| 36 | Shule ya Sekondari Lesoit | Kiteto DC-MANYARA | Ujenzi upo katika hatua ya kumalizia |
| 37 | Shule ya Sekondari Loiboriret | Simanjiro DC-MANYARA | Ujenzi upo katika hatua ya kupaua |
| 38 | Shule ya Sekondari Yaeda Ampa | Mbulu DC-Manyara | Ujenzi upo katika hatua ya kumalizia |
| 39 | Shule ya Sekondari Vumari | Same DC-KILIMANJARO | Ujenzi upo katika hatua za awali. |
| 40 | Shule ya Sekondari Micheni | Mafia DC-PWANI | Ujenzi upo katika hatua ya kupaua |